# Nipashe

Ijumaa Mei 15, 2020 • Tanzania 1,000/- Kenya 100/-

MWANGA WA JAMII

ISSN 0856 • Na. 0580232

www.ippmedia.com



The Guardian digital  nipasheTZ  nipasheTZ  nipasheTZ  0745 700710




## Ndege kuleta wataalamu wa afya, vifaa nchini leo

UKURASA 2



Asasi TCRS ilivyowekeza maarifa kwa Machinga Moro 'wakamea' Ukurasa 13

BUFE

IJUMAA MEI 15, 2020 Nipashe

BIASHARA, UCHUMI NA FEDHA

Daraja mwokozi Tambani Mkuranga labomoka tena Ukurasa 14

BIASHARA

BOSI WA JPM NYANZA:

Yuleyule na 'hapa kazi tu' hajabadilika hata chembe

• Alipaisha uzalishaji akiamini'mwizi tumtumbue' kiwandani akazijua 'dili' • Alikesha siku 3 • Mameneja: Wa watu, hapindishi ukweli

Na Anthony Gervas, MWANZA

"HAPA kazi tu!" imekuwa kaulimbiu yake na falsafa yake kikazi. Ni kweli, tangu kumfahamu akiwa katika ulingo wa kisiasa ndani ya Baraza la Mawaziri, wasifu wa uchapa kazi wake umebaki kuwa nembo inayomtambulisha.

Wizara ya Ujenzi, alama ya mafanikio yake kiutendaji, takwimu na matendo yake yalifanyika ndani ya kumbukumbu ya kichwa kwa kiasi kikubwa, aliorodhesha takwimu mbalimbali na marejeo ya maandiko yalichukua nafasi ya ushahidi au uhakiki pekee. Kuna wakati ni hadi katika majibu ya papo kwa hapo bungeni.

Ni simulizi inayoenda mbali katika umahiri, tija na mageuzi makubwa ndani ya wizara nyinginezo alikopitia, ikiwamo yenye dhamana na Ardhi, pia Uvuvi. Ni ushuhuda unaoendelea kuonekana 'hapa kazi tu' katika zama za Serikali ya Awamu ya Tano.

Wasifu mwingine wa kikazi, kitaaluma ni mwalimu na mwansayansi ambaye mfumo wake wa uongozi kimatendo ni mchumi aliyetimia, kwa maana ya kuokoa hasara kwa kile anachokisimamia na wakati huohuo, kuongeza tija katika anachokizalisha.

Chama cha Wachumi cha Marekani (AEA), kinatoa tafsiri ya uchumi kwamba ni elimu ya matumizi ya rasilimali katika mazingira ya uhaba unaiokabiliwa na mahitaji mengi, yanayofanyiwa uamuzi sahihi kukidhi mahitaji kipaumbele

John Masalu ambaye ni Meneja Shughuli wa Ushirika Nyanza, aliyefanya kazi na Rais Dk. John Magufuli. PICHA: ANTHONY GERVAS

"Hapo ndipo nilipoanza kumfahamu, sababu na mimi niliajiriwa mwaka 1989 Ushirika Nyanza.

kilichopo mbele yao.

Kimsingi, ikiangaliwa ndio falsafa ya uamuzi mara nyingi anafanya Rais Dk. Magufuli katika utendaji wake wa kila siku, kila rasilimali ikiwamo muda ni kipaumbele kwake.

Hayo ndiyo yanashuhudia katika mengi ya maisha ya kila siku nchini serikalini, hata baadhi ya tija za barabara za ndani ya miji nchi kujengwa.

Lakini kama wanavyosema Waswahili "usione vinalelea, vimeundwa." Nipashe ilifanya 'kiguu na njia' hadi kwenye 'nyayo' zake

alikopitia kabla ya utumishi wa kisiasa, kudodosa, je, ni Dk. Magufuli huyu huyu tuliye naye katika wajihi huu wa 'hapa kazi tu?'

Hapo ni katika Ushirika wa Nyanza, jijini hapa Magufuli wakati huo kabla hajawa na sifa ya daktari, alikoajiriwa katika nafasi ya Mkemia Mkuu wa Viwanda, alikotumia taaluma ya kemia, ambayo leo hii ina madarasa iliyoongezewa, akitumia na pacha wake, hisabati na ualimu, kazi yake ya awali.

Mzee Enock Masele, Meneja mstaafu wa Ushirika wa Nyanza, hakuwa mchoyo wa ufafanuzi, aki-

anza kuanika wasifu wake kupitia matokeo ya kazi zake, kwa kueleza ushuhuda wa aliyofanya:

"Wakati hajaajiriwa Magufuli, mafuta viwandani tani moja ya mbegu za pamba ilitoa debe sita tu za mafuta, lakini alipoingia katika nafasi hiyo, alisimamia na kuanza kufanya majaribio ya kuzalisha mafuta hayo ili kuhakiki tani moja ya mbegu inazalisha debe ngapi za mafuta.

"Aligundua tani moja ina uwezo wa kuzalisha mafuta kuanzia debe tisa hadi kumi. Uzalishaji huo wa mafuta ulikuwa ukitegemea ubora wa mbegu na hivyo aliweza kugundua kumbe kulikuwa na wizi wa mafuta uliokuwa ukifanywa na mameneja wa viwanda hivyo wakanda.

"Aliweza kuwadhibiti (watumishi wadokozi) vikali. Alikuwa akilazimika kukesha kiwandani hadi ahakikishe mbegu zilizozalishwa kulingana na ubora wake zitatoa mafuta kiasi gani," anasimulia Mzee Masele, anayedai kumfahamu vyema Magufuli, msaidizi wake mwandamizi kazini na kijana wake.

Ni mwendelezo wa hoja ambayo, John Masalu, Meneja Shughuli wa Ushirika Nyanza, anaunga mkono kufahamu, naye akiendeleza simulizi ya dokezo la Mzee Masalu, kwa ufafanuzi wake mpya:

"Alianza kufuatilia matokeo ya uzalishaji wa mafuta ya pamba viwandani (ginery) na kuanza kufanya majaribio kilo 1000 ya mbegu ya pamba inaweza kutoa kuzalisha mafuta debe ngapi, mashudu kiasi gani na uchafu wake kiasi gani, mpaka ahakikishe ndipo aondoke kiwandani.

"Magufuli ni mwalimu wa Hesabu na Kemia! Hakupenda uongo wala wizi ndiyo maana hata sasa anaendeleza yale mazuri na msimamo wake wa kuchapa kazi alivyotoka nao Nyanza. Ni mtu asiyejaribiwa, mwenye kumbukumbu

INAENDELEA UK.12

UKURASA 11

TISHIO LA CORONA

# Tume yashtushwa wagonjwa kuzuiwa

**MADAKTARI**, wauguzi walalamikiwa kulazimisha wagonjwa wote wapimwe corona kwanza...*Endelea ukurasa 2*



Baadhi ya wakazi wa Nakonde nchini Zambia, wakipita katika njia isiyo rasmi, katika mpaka wa Tanzania na nchi hiyo uliofungwa, wakivuka kwenda eneo la Tunduma, mkoani Songwe jana, kujipatia mahitaji mbalimbali. **PICHA: MANUEL KAMINYOGE**

## SERIKALI KUFYEKA KODI, ADA ZA MIFUGO

UKURASA 3

## Mbowe mikononi mwa polisi

UKURASA 2

## BAA LA CORONA



Unapojikinga na virusi vya corona, hakikisha usalama wako unapofanya shughuli mbalimbali zinazofaa kwa kiwango cha afya yako kama inavyoelekezwa na watalaamu wa afya. Shirika la Afya Duniani (WHO), linashauri kuwa unaweza pia kufanyakazi za nyumbani kama njia ya kukuweka 'fit'.

* **Epuka mikusanyiko ya watu**
* **Nawa mikono kwa sabuni na maji yanayotiririka**
* **Epuka kusalimiana kwa kushikana mikono na kukumbatiana**
* **Ukipiga chafya au kukohoa, ziba mdomo**


Scan Hapa




Fungua App ya QR code Reader kisha scan kupakua APP yetu

Google Play  App Store



**MICHEZO** **UTATA MABILIONI YA FIFA WAANIKWA** UK.24

**MAONI, KATUNI UK.6**

# Tume yashtushwa wagonjwa kuzuiwa

**Na Salome Kitomari**

TUME ya Haki za Binadamu na Utawala Bora (THBUB) imeeleza kusikitishwa na taarifa ya vitendo vinavyofanywa na baadhi ya madaktari na wauguzi wa Hospitali ya Rufani ya Mkoa ya Mwananyamala jijini Dar es Salaam, vya kuwanyanyapaa na kuwasumbua wagonjwa wanaoenda kupata matibabu.

Aidha, Tume hiyo imesema wagonjwa hao wanatakiwa kufanya vipimo vya virusi vya corona kabla ya kuanza kupata matibabu.

Taarifa ya Tume iliyotolewa na Mwenyekiti wake, Jaji mstaafu Mathew Pauwa Mhina Mwaimu, ilieleza kuwa:

"Tume imesikitishwa na jambo hilo kwa sababu kila mwananchi ana haki ya kufurahia haki ya afya kwa kupata matibabu mazuri na ya uhakika. madaktari na wauguzi wanapaswa kutambua kuwa sio kila mgonjwa ana maambukizo ya corona.

"Tume inaamini vitendo vya namna hiyo ni ukiukwaji wa haki ya afya kwa wananchi, na vinaweza kusababisha wagonjwa kupoteza maisha."

Hata hivyo, THBUB imempongeza Waziri wa Afya, Maendeleo ya Jamii, Jinsia na Watoto, Ummy Mwalimu, kwa kuchukua hatua za haraka za kukemea vitendo hivyo vya baadhi ya madaktari na wauguzi, ambavyo vinaweza kuchafua taswira nzuri ya sekta ya afya na jitihada mbalimbali zinazochukuliwa na Serikali.

Kadhalika, Tume inaiomba Serikali iendelee kuhakikisha hospitali zinaendelea kutoa huduma nzuri kwa wagonjwa ili kuepusha malalamiko yasiyo ya lazima.

Aidha, Tume imeiomba Serikali kufanya uchunguzi wa kina ili kubaini chanzo cha vitendo hivyo vinavyofanywa na baadhi ya madaktari na wauguzi ili kuvitafutia ufumbuzi wa haraka.

**ALICHOBAINI WAZIRI UMMY**

Hivi karibuni, Waziri Mwalimu, alifanya ziara ya kushtukiza katika Hospitali ya Mwananyamala na kukuta wagonja wengi wakisubiri huduma baada ya kupigwa danadana kwenye hospitali mbalimbali za Jiji la Dar es Salaam na kutakiwa kupima corona kwanza kabla ya huduma.

"Tunaaambiwa tuende Palestina saa nane usiku hawapigia X ray, tumerudi Magomeni wanatuambia mpelekeni mgonjwa wenu nyumbani, tunakuja naye hospitalini Magomeni wanatuambia tuende tena Mwananyamala, tunakuja hapa tunaambia turudi tena Magomeni,mgonjwa wtu huyu hapa na hali yake ni mbaya," alisema mmoja wa ndugu wa mgonjwa.

Mwingine alimwambia Waziri: "Tangu saa 12 asubuhi tuko hapa hatujapata huduma, tunaomba huduma wangetuokoa sisi turudi nyumbani tunawatoto ili tusijazane hapa."

"Tulifika hapa baba ana sukari wakasema hawana kipimo cha sukari, tumenunua kipimo wakakataa, wakasema hawamshiki mgonjwa hadi apimwe corona, tukaaomba tuelekezwe pa kumpima corona, lakini hawajatoa jibu, tangu asubuhi mgonjwa wetu yupo hapa hajapata huduma," alisema mmoja wa ndugu.

Kutokana na vilio hivyo, Waziri Ummy alionyesha kukasirika na kumwambia "Mganga Mkuu hiki mnachokifanya mjue mtakuja kuua watu, mtu ameata ajali tangu jana usiku hadi sasa hajapata huduma, mtu ana sukari unamwambia apime kwanza corona."

Alisema madakitari na wahudumua wa afya wanapaswa kuendelea kutoa huduma kwa uangalifu mkubwa kwa kuwa maisha lazima yaendelee.

"Watoa huduma za Afya wa Serikali na binafsi acheni kunyanyapaa wagonjwa, mgonjwa amekuja na tatizo la sukari mtibuni sukari, mnaleta ya corona... hayo ni mambo mengine, mtamuua mtu si kwa sababu ya corona bali kwa sababu hamkumpa matibabu ya sukari," alisema Waziri.



Mafundi wakiendelea na ujenzi wa daraja la juu la mpishano la Ubungo (Ubungo Interchange), katika makutano ya Barabara za Morogoro, Sam Nujoma na Mandela jijini Dar es Salaam jana. **PICHA: MIRAJI MSALA**

# Mbowe mikononi mwa polisi

**Na Romana Mallya**

CHAMA cha Demokrasia na Maendeleo (Chadema), kimesema Mwenyekiti wake, Freeman Mbowe, amehojiwa na Jeshi la Polisi Mkoa wa kipolisi Kinondoni baada ya jana kutakiwa kuripoti kituo cha polisi.

Msemaji wa chama hicho, Tumaini Makene, aliliambia Nipashe jana kuwa, baada ya Mbowe kutangaza kufanya mkutano na waandishi wa habari kwa njia ya mtandao saa 5:00 asubuhi, jeshi hilo lilimtaka kuripoti kwake kwa ajili ya mahojiano.

"Mbowe aliitwa Kituo cha Polisi Oysterbay kwa mahojiano baada ya kutangaza kufanya mkutano na walipomuhoji, walimwachia," Makene alisema bila kubainisha mambo aliyohojiwa kiongozi huyo.

Jana asubuhi, ilitangazwa na Chadema kupitia Makene kwamba majira ya saa 5:00 asubuhi, Mbowe alitarajiwa kuzungumza na waandishi wa habari na umma kupitia mtandao, lakini muda mfupi baada ya taarifa hiyo, chama hicho kilitangaza kusitisha mkutano huo baada ya kiongozi wake huyo kupokea wito wa kuhitajika kituo cha polisi.

Makene alisema Mbowe alitii wito huo uliomtaka kuripoti Kituo cha Polisi Oysterbay kwa Mkuu wa Upelelezi Mkoa wa Kipolisi Kinondoni na mkutano huo kuahirishwa.

Juhudi za Nipashe kumtafuta Kamanda wa Polisi wa Mkoa wa Kipolisi Kinondoni na Kamanda wa Polisi Kanda Maalum ya Dar es Salaam kuzungumzia suala hilo, hazikuzaa matunda baada ya wawili hao kutopokea simu.

## Ndege kuleta watoa huduma kibinadamu, afya nchini leo

**Na Mwandishi Wetu**

NDEGE ya abiria yenye wafanyakazi wanaotoa huduma za kibinadamu na afya inatarajiwa kutua nchini leo ikitokea Addis Ababa, Ethiopia.

Ndege hiyo ni ya kwanza ya aina yake tangu safari za ndege za kibiashara zilipositishwa kuja Tanzania kwa lengo la kupambana na janga la Covid-19.

Taarifa iliyotolewa na Shirika la Mpango wa Chakula Duniani (WFP), imesema huduma hiyo ya abiria wa anga, ikiwa inaendeshwa na shirika hilo, ni sehemu ya mfumo wake ulimwenguni katika kutoa misaada ya ugavi kupambana na Covid-19.

"Huduma hii itahakikishia mashirika yanayotoa huduma za kibinadamu kwamba yanaweza kutoa huduma kufikisha watu na mizigo inayohitajika kwa misaada endelevu ambayo mamilioni ya watu wahitaji ulimwenguni kote," ilisema taarifa hiyo.

Mfumo unaounganisha anga unategemea hasa vituo vya usaidizi wa misaada ya kibinadamu ulimwenguni vilivyopo Guangzhou (China), Liège (Ubelgiji) na Dubai (UAE), vifaa vinazalishwa na vituo vya kikanda nchini Ethiopia, Ghana, Afrika Kusini, Malaysia, Panama na Dubai.

Taarifa hiyo ilisema ndege hufanya kazi baina ya vituo vya kimataifa na vya kikanda, na ndege ndogo zinasambaza mizigo na wafanyakazi wa huduma za kibinadamu katika nchi maalumu, ikiwamo Tanzania.

Ilisema huduma zitakapo imarika, WFP inatarajia kuimarisha safari za kawaida katika maeneo muhimu duniani.

"WFP ni Shirika la mstari wa mbele Umoja wa Kimataifa katika ugavi, ambalo lina jukumu muhimu kuzisaidia serikali na jamii kwa ujumla kuhakikisha misaada ya kibinadamu inafika mahali inapohitajika," alisema Michael Dunford, Mwakilishi Mkazi wa WFP Tanzania. "Uzoefu wetu katika uendeshaji wa shughuli za ugavi umetupatia fursa ya kuweka mipango yetu vizuri ili kutoa huduma za ugavi kwa ujumla kusaidia huduma za kibinadamu na afya ulimwenguni."

Taarifa hiyo iliongeza kuwa WFP inatarajia kwa Tanzania kutakuwapo safari hizo za ndege kwa ajili ya wafanyakazi wanaotoa huduma za kibinadamu na afya zitakazofanyika kila wiki.

Ndege itakapowasili, abiria watafuata masharti yaliyowekwa na Serikali ya Tanzania kwa kuwatenga.

## HABARI KITAIFA



Mkuu wa Mkoa wa Morogoro, Loata Ole Sanare (kulia), akimpa pole Sarah Athumani mkazi wa kijiji cha Mangae, wilaya ya Mvomero mkoani humo juzi, aliyefiwa na mumewe kwa kuuawa na tembo. **PICHA: FRANK KAUNDULA**

# Benki zafurahia uamuzi wa BoT

**Na Salome Kitomari**

TAASISI za fedha zimesema kuwa zimefurahishwa na uamuzi wa Benki Kuu ya Tanzania (BoT), kupunguza riba, amana, hatifungani na dhamana kwa mikopo inayotolewa kwa benki nchini.

Akizungumza na Nipashe kwa njia ya simu, Mwenyekiti wa Umoja wa Benki Tanzania (TBA), Abdulmajid Nsekela, alisema ahueni hiyo itasaidia kwenye mikopo inayochukuliwa na benki na wateja pia.

"Kama benki tumefurahi sana maamuzi ya Benki Kuu, kwa kuwa itaongeza mzunguko wa fedha sokoni kwa benki kupata uwezo wa kutoa mikopo kwa sekta binafsi, kutoa uhuru kwa benki kuangalia waathirika," alisema na kuongeza:

"Sekta zenye matatizo ya muda kama utalii, zinaweza kupewa kupindi cha uangalizi, inasaidia mteja mwenye mkopo ambaye hajapata mapato tangu kuanza kwa corona kuendelea kujiendesha."

Nsekela ambaye ni Mkurugenzi Mtendaji wa Benki ya CRDB, alisema auheni hiyo itawasaidia wateja kukopa zaidi ikiwamo kuongeza wigo wa kuwakopesha watu na benki zitazokopa kutoka BoT kwa riba ndogo na hivyo kuongeza fedha kwenye mzunguko.

**"Kwa mtazamo wangu tumechelewa kwa kuwa ilipaswa kuokoa mapema kilichopaswa kupotea, uchumi hausubiri na kilichopaswa kufanyika ni kuanza tangu mwezi Machi, mwaka huu corona ilipoingia," alisema.**

Kwa mujibu wa Nsekela, wateja wazuri wenye mikopo ambao sekta zao zimeathiriwa na corona, wana changamoto ya kupungua kwa mapato na wengine kufunga biashara.

Vile vile, alisema wateja wenye changamoto mbalimbali ni wakati mzuri wa kuongea na benki zao ili kuonyesha malengo ya sasa na baadaye baada ya ugonjwa, na ziwe karibu kujadiliana suala hilo.

Naye, Mchumi Prof. Honest Ngowi, alisema kilichofanywa na BoT ni sera pana za kifedha, ambazo huchukuliwa wakati wowote wa mtikisiko wa kiuchumi ambayo inataka kuwapo kwa miitikio ya kisera itakayochochea uchumi.

"Ni muhimu kuwa na mwitikio wa mazingira rafiki, wezeshi ili sekta binafsi ziendelee kukopa, ili kampuni ziweze kuendelea na biashara na baada ya corona kutakuwa na uponyaji ili ziweze kuendelea kuimarika," alifafanua.

"Kwa mtazamo wangu tumechelewa kwa kuwa ilipaswa kuokoa mapema kilichopaswa kupotea, uchumi hausubiri na kilichopaswa kufanyika ni kuanza tangu mwezi Machi, mwaka huu corona ilipoingia," alisema.

# Serikali kufyeka kodi, tozo mifugo na uvuvi

**Na Gwamaka Alipipi, DODOMA**

WAZIRI wa Mifugo na Uvuvi, Luhaga Mpina, amesema serikali itazifanyia tathmini kodi, tozo na ada mbalimbali ambazo zimekuwa kero kwa wazalishaji na wafanyabiashara wa mifugo na mazao, ili kuzifuta na kuzifanyia marekebisho.

Alitangaza neema hiyo jana bungeni jijini hapa, alipowasilisha makadirio na mapato na matumizi ya wizara yake kwa mwaka ujao wa fedha, akiliomba Bunge kuidhinisha Sh. bilioni 66.82.

Waziri Mpina alisema kutokana na malalamiko ya wadau juu ya kiwango kikubwa vya kodi, ada, ushuru na tozo, wizara yake imesikia kilio hicho na inatarajia kufanya mapitio ya kanuni zake.

Alisema mwaka ujao wa fedha, wizara inatarajia kufanya maboresho ya ada mbalimbali za leseni za wavuvi kwa lengo la kuwapa unafuu wavuvi.

"Wizara imesikia kilio cha wavuvi na kufanya maboresho ya ada mbalimbali za leseni. Mabadiliko haya yataonekana katika muswada wa Sheria ya Fedha ya Mwaka 2020/2021.

"Uboreshaji wa ada za leseni na tozo za uvuvi unalenga kuhamasisha uwekezaji katika sekta ya uvuvi na kukuza biashara ya samaki na mazao yake," alisema.

Waziri Mpina pia alisema katika mwaka 2019/2020, wizara imetatua migogoro mikubwa 11 kati ya 17 baina ya wafugaji na watumiaji wengine wa ardhi katika mikoa ya Pwani, Dodoma, Morogoro, Ruvuma, Mwanza na Geita.

Vilevile, waziri huyo alisema tangu machinjio ya Dodoma yalipokabidhiwa kwa Kampuni ya TMCL mwaka 2008, utendaji wake umekuwa siyo wa kuridhisha.

Alisema usimamizi dhaifu na ubadhirifu wa fedha katika machinjio hayo, umesababisha serikali kupata hasara ya Sh. bilioni 42.28 kwa kipindi cha miaka 11.

"Kutokana na udhaifu huo wa uendeshaji na uchakavu wa machinjio, Wizara ya Mazingira ya UAE (nchi za Falme za Kiarabu) inayosimamia ubora wa nyama, iliifutia machinjio ithibati ya kuuza nyama katika nchi za UAE," alibainisha.

Waziri Mpina pia alisema idadi ya watumishi wa ugani katika sekta ya mifugo bado ni ndogo kulinganishwa na mahitaji.

Alibainisha kuwa mahitaji ya wataalamu wa ugani wa mifugo kwa sasa ni 17,848, lakini idadi ya wagani wa mifugo waliopo kwa sasa katika mikoa na mamlaka za serikali za mitaa ni 3,795, hivyo kuwa na upungufu wa wagani 14,053.

Alisema katika mwaka 2019/2020, juhudi za kuimarisha ukusanyaji wa maduhuli kutokana na uvuvi wa Bahari Kuu zilifanyika ikiwa ni pamoja na serikali kuondoa tozo ya Dola za Kimarekani 0.4 kwa kilo ya samaki.

Kiongozi huyo wa wizara alisema kuwa, baada ya serikali kuondoa tozo hiyo, mashirika ya meli kutoka nchi za Ufaransa, Hispania na Shelisheli yalileta maombi ya leseni za uvuvi ili kufanya uvuvi katika Bahari Kuu.

Hata hiyo, Waziri Mpina alisema kuwa, baada ya kutokea kwa mlipuko wa ugonjwa wa homa ya mapafu inayosababishwa na virusi vya corona, mashirika hayo yametoa taarifa za kusitisha nia hiyo.




**Bonite Bottlers Ltd** inayo furaha kuwaletea **Maji ya Kilimanjaro katika ujazo mkubwa wa LITA 6, LITA 12 na LITA 18.9.** Tumewekeza katika mitambo ya kisasa ya kuzalisha maji katika ujazo mkubwa ili kuwawezesha wateja, wanywaji na wadau wetu kupata maji kwa ajili ya matumizi ya majumbani, maofisini na kwenye taasisi mbalimbali.

**UPATIKANAJI:-**

- Maji ya Kilimanjaro katika ujazo mkubwa yanapatikana kwenye depoti zetu zote zilizoko mikoani, maduka na wauzaji wa jumla nchi nzima.
- Kwa Wateja wetu wa Mkoa wa Dar es Salaam, unaweza kununua maji ya kunywa ya Kilimanjaro ukiwa nyumbani kwa njia ya mtandao kupitia makampuni ya usambazaji bidhaa tunayoshirikiana nayo ambayo ni Shoponline Tanzania **www.shoponline.co.tz** na Piki Deliveries **www.piki.co.tz** .

Ni matumaini yetu mtaendelea kutuunga mkono kwa kuburudika na maji kutoka kilele cha Afrika.

**KWA MAWASILIANO ZAIDI:**

**Moshi:** +255 755851170 au +255 27 2754422/7, **Arusha:** +255 756339532 au +255 27 2544876, **Dar: +255 754635988 au +255 22 700450/655, Morogoro:** +255 782546090, **Dodoma:** +255 787495439, **Karatu:** +255 757673123, **Babati:** +255 765459199, **Singida:** +255 755271963, **Tanga:** +255 763407979, **Mbeya:** +255 757266235, **Mwanza:** +255 742099191, **Nzega:** +255 746031412

**MAJI YA KUNYWA YA KILIMANJARO NI MAJI YA KUAMINIKA KILA SIKU!**

# Polisi yakamata magari 6, ofisa usalama 'feki'

**Na Paul Mabeja, DODOMA**

JESHI la Polisi mkoa wa Dodoma linamshikilia Shaban Wisandala (32), mkazi wa Medeli jijini Dodoma, kwa kujifanya ofisa usalama wa taifa, pamoja na magari sita yaliyokamatwa kutokana na kusadikiwa kuwa ni ya wizi.

Akizungumza na waandishi wa habari jijini hapa Kamanda wa Polisi, Mkoa wa Dodoma, Gilles Muroto, alisema Mei 13, mwaka huu, Mtaa wa Medeli, Kata ya Tambukareli alikamatwa mtuhumiwa huyo akijifanya ofisa usalama wa taifa.

Alisema mtuhumiwa huyo amekuwa akijitambulisha kwa watu mbalimbali, kuwatishia maisha na kudai fedha kwa vitisho akitishia kuwakamata, kuwaharibia kazi na kutumia vibaya majina ya viongozi wa serikali wakati akidai fedha.

"Huyu mtuhumiwa tunamshikilia na bado tunamuhoji kwa kina na baadaye tutampeleka mahakamani kwa ajili ya hatua zaidi za kisheria," alisema Kamanda Muroto.

Akizungumzia magari yaliyokamatwa alisema, Mei 10, mwaka huu majira ya 10:00, Kijiji cha Mbande, Kata ya Sejeli, Wilaya ya Kongwa, barabara kuu ya Morogoro na Dodoma, lilikamatwa gari namba T936 Toyota Land Cruiser VX, rangi nyeupe.

Muroto, alisema kuwa katika uchunguzi wa gari hilo limegundulika kutofautiana namba na taarifa zilizopo kwenye kadi.

Alisema gari hilo lilikuwa likiendeshwa na Ramadhani Sekiondo (31), mkazi wa Magomeni Mikumi Dar es Saalam baada ya kukabidhiwa na mtu asiye mfahamu.

"Huu ni mtandao wa wizi wa magari tutaufutilia kwa kina na kuushughulikia bila huruma na sheria itachukua mkondo wake," alisema Kamanda Muruto.

Pia alisema kuwa magari mengine mawili yalikamatwa Mei 11, mwaka huu mtaa wa Area 'A' Kata ya Kizota jijini Dodoma, yakiwa yamefungiwa ndani ya nyumba yasiyo na namba za usajili yakitumia namba za chassis ambayo ni Toyota Harrier Chassis namba MCU310001691, injini namba 1MZ1589700 na Toyota IST chassis namba NCP600209833, injini namba 2MZ3578179.

"Katika uchunguzi wa awali imegundulika kuwa hayana kumbukumbu zozote na yaliingia nchini bila kibali, uchunguzi zaidi unaendelea kwa kushirikiana na Interpol kubaini taarifa za kina za magari hayo na mtuhumiwa Omari Chilipachi (29), mkazi wa Sinza, Dar es Saalam, anahojiwa na polisi kuhusu tukio hilo," alisema Kamanda Muroto.

Pia, Muroto alisema Mei 11, mwaka huu huko Area A, Kata ya Kizota, lilikamatwa gari aina ya Land Rover Discovery lenye namba za usajili wa nchi ya Afrika Kusini SJV576 GP.

Alifafanua kuwa kadi ya gari hilo inasomeka chassis SALLAAA135A339616, ambayo zinatofautiana na zilizopo katika gari ni 04905312103030507 1757 na hazipo katika mfumo wa usajili wa magari.

"Uchunguzi zaidi unafanyika ili kubaini ukweli wa uhalali wa gari hilo na mtuhumiwa Jamal Rashid (28), mkazi wa Area A, anahojiwa na jeshi hilo juu ya uhalali wa gari hilo," alisema.

Katika tukio jingine Mei 12, mwaka huu huko Nzuguni, polisi ilikamata gari aina ya Toyota Alphard lenye kadi namba za usajili T384 DMU lenye chassis namba ANH100038956, injini namba 2AZ1184313 rangi ya Silver.

"Katika uchunguzi wa awali imebainika kuwa shassis ANH100030547 na ingini ZNZ 0860988 halisi kwenye gari zinatofautiana na kadi ya gari hilo aidha rangi ya gari hiyo ni nyeusi siyo Silver kama linavyoonekana," alieleza Muroto.




Kamanda wa Polisi Mkoa wa Dodoma, Gilles Muroto, akionyesha magari kwa waandishi wa habari mkoani humo jana, yaliyokamatwa hivi karibuni na jeshi hilo kwa madai ni mali za wizi. **PICHA: PAULO MABEJA**

## Majaliwa aiagiza Tanesco mradi umeme Nyerere

**Na Mwandishi Wetu**

WAZIRI Mkuu, Kassim Majaliwa, amekagua maendeleo ya ujenzi wa mradi wa kufua umeme wa Julius Nyerere (JNHPP) utakaozalisha Megawati 2,115 na amemwagiza Mkurugenzi Mtendaji wa Shirika la Umeme Tanzania (Tanesco), Dk. Tito Mwinuka, ausimamie ili ukamilike kwa wakati.

Vilevile, Waziri Mkuu amemwagiza mkandarasi anayejenga mradi huo aukamilishe kwa wakati kwa sababu imebainika kuwa mvua zinazoendelea kunyesha nchini haziathiri utekelezaji wa ujenzi huo.

Waziri Mkuu alitoa maagizo hayo jana akiwa katika ziara ya kukagua hatua za utekelezaji wa mradi huo. Alisema ameridhishwa na maendeleo ya ujenzi wa mradi huo mkubwa wa kimkakati.

"Nimetembelea eneo la mradi na kujionea shughuli zote zinazoendelea, kazi inayofanyika ni ya uhakika, huku kukiwa na matumaini makubwa ya kukamilisha mradi mapema kabla ya muda uliopangwa."

Mradi wa umeme wa maporomoko ya maji ya Mto Rufiji unajengwa na kampuni ya Arab Construction kwa pamoja na kampuni ya Elsewedy Electric zote za kutoka nchini Misri. Mradi huo unatarajiwa kuzalisha Megawati 2,115 ambazo zitaingizwa kwenye grid ya Taifa na kuifanya nchi kuwa na umeme mwingi na wa uhakika.

Mbali na kuliwezesha Taifa kuwa na umeme wa uhakika, pia mradi huo umewezesha kupungua kwa changamoto ya ajira baada ya Watanzania wengi wakiwamo makandarasi kupata ajira za kudumu na za muda mfupi.

Kukamilika kwa utekelezaji wa mradi huo, kutaiwezesha Tanzania kuzalisha kiasi kikubwa cha umeme kitakachosaidia kutekeleza miradi mikubwa ya kimkakati ikiwamo ujenzi wa uchumi wa viwanda na mradi wa reli ya kisasa.

# Waajiri wapewa mbinu kukabili athari za corona

**Na Elizabeth Zaya**

WANATAALUMA na wafanyabiashara wametoa maoni na mbinu za kusimamia biashara zao bila kusababisha madhara makubwa katika biashara zao kipindi hiki cha mlipuko wa virusi vya corona vinavyosababisha homa kali ya mapafu.

Imeelezwa kuwa sekta ya biashara imeathirika kwa kiasi kikubwa kutokana na mlipuko wa ugonjwa huo kwa kuwa inategemea kwa kiwango kikubwa rasilimali watu katika uzalishaji na masoko pia.

Pia, utalii, huduma za hoteli, usafirishaji na hata huduma za kijamii nazo zinasumbuka kukabiliana na utamaduni wa kutokujumuika moja kwa moja.

Kwa kutambua baa hilo, Kampuni ya Brighter Monday Tanzania, iliamua kuchukua hatua kukabiliana na athari zilizoibuliwa kutokana na mlipuko wa corona kwa kuandaa mkutano wa mtandaoni ambao uliwaleta pamoja jumla ya maofisa rasilimali watu na waajiri 135 kutoka Tanzania na nje ya mipaka ya nchi, ili kujadili umuhimu wa rasilimali watu katika kuhakikisha uendelevu wa biashara.

Wakati wa mkutano huo, wanataaluma na wafanyabiashara walitoa maoni na mbinu za kusimamia biashara zao bila kusababisha madhara makubwa katika biashara zao wakati huu wa maambukizo ya virusi hivyo.

Wazungumzaji wakuu katika mkutano huo waliwasihi waajiri na waajiriwa kujitahidi kuendana na hali ya ugonjwa wakati wakikabiliana na mabadiliko katika biashara zao bila kuathiri uzalishaji.

Mosses Raymond, mtaalamu wa rasilimali watu ambaye alikuwa mzungumzaji katika mkutano huo, alisisitiza umuhimu wa waajiri kutumia mbinu mpya za kufanya usaili wa wataalamu hasa kwa kuzingatia kwamba mlipuko wa corona umebadilisha kwa kiasi kikubwa mbinu zilizozoeleka katika usaili.

"Kwa kuzingatia kwamba tunalazimika kuendana na utamaduni mpya wa kufanya kazi na biashara, tunapaswa pia kukumbuka kwamba wataalamu ni hitaji muhimu zaidi kwa biashara zote, hivyo tunapaswa kutumia majukwaa ya mtandaoni kuimarisha rasilimali watu tulizonazo na kujipatia rasilimali watu nyingine.

"Tunaweza kutumia fursa na nyenzo stahiki zinatolewa na BrighterMonday Tanzania kufanya usaili na kuwezesha uendelevu wa biashara zetu," Raymond alishauri.

Mzungumzaji mwingine katika mkutano huo, Heather O'Shea, Mkuu wa Kitengo cha Rasilimali Watu wa ROAM - Afrika, aliwasihi waajiri na maofisa rasilimali watu kuibua ubunifu mpya utakaowawezesha watendaji kufanya kazi kama timu na kuendelea kuwa na afya njema wakati wakifanya kazi wakiwa nyumbani.

Heather alikazia umuhimu wa waajiri kuongeza jitihada katika kukabiliana na athari zinazowakabili waajiriwa wakiwa nyumbani ili kufanya kazi kama timu na kuongeza uzalishaji.

Ezra Kimondo, mtaalamu wa usimamizi wa uzalishaji wa Brighter Monday, alitambulisha mfumo wa kidigitali kupima ustadi wa mwajiriwa (Skills Assessment Tool), ambao wameubuni kwa lengo la kuwawezesha waajiri kufanya usaili mtandaoni.

Mkurugenzi Mkuu wa Brighter Monday Tanzania, Reshma Bharmal-Shariff, aliwashukuru washiriki wa mkutano huo na kuwahakikishia kwamba kampuni hiyo itaendelea kuibua mbinu mbalimbali za kuboresha usimamizi wa rasilimali watu hasa kwa lengo la kukabiliana na ugonjwa wa corona.

## Masauni azindua Bodi ya Parole

**Na Renatha Msungu, DODOMA**

NAIBU Waziri wa Mambo ya Ndani, Hamad Masauni, amezindua rasmi Bodi ya Parole huku akiwataka kutekeleza wajibu wao ipasavyo kama Rais Dk. John Magufuli alivyowaamini na kuwapa jukumu hilo.

Jumla ya wafungwa 5,535 wameachiwa huru kupitia mpango wa Parole na kwenda uraiani kuendelea na majukumu yao ya kila siku.

Akizungumza na uzinduzi huo, Masauni alisema serikali imewaamini hivyo na wao waende kufanya kazi bila kuleta malumbano kwa ajili ya kuendeleza gurudumu hilo ambalo wamekabidhiwa.

Alisema ili kuhakikisha jamii inashilikishwa kikamilifu katika kurekebisha wahalifu kwa kuwapa wafungwa fursa ya kutumika sehemu ya adhabu zao wakiwa nje ya Magereza kwa usimamizi.

"Tunaona Parole inavyofanya kazi zake hivyo endeleeni kuchapa kazi ili kumsaidia Rais katika majukumu yake," alisema Masauni.

Alisema nyenzo kubwa ya msingi ni katika mambo matatu ambayo ni uwelewa, na dhana yenyewe, umuhimu katika jamii, uwelewa wa sheria na utekelezaji.

Alisema dhima na dhana ya mpango wa Parole imeanza kutekelezwa nchini kwa takribani miaka 21 na Bodi ya Taifa ya Parole ya awamu ya sita zimeshiriki kikamilifu na kufanikisha jumla ya wafungwa 5,535 kuachiliwa kwa mpango huo.

Aliwaasa wafungwa ambao wamebahatika kupata fursa ya kunufaika na mpango wa Parole kuwa na nidhamu na kukubali mafunzo ya urekebishaji wanayopata.

"Naomba wafungwa mlioachiwa kwa mpango wa Parole kubadilika tabia ili kuwafundisha na wengine," alisema Masauni.

Naye Mwenyekiti wa Bodi ya Parole, Dk. Augustino Mrema, alisema ataifanya kazi hiyo kwa weledi ili kumsaidia Rais katika jukumu ambalo amempa.

Alisema yeye na wajumbe wengine wa bodi hiyo wamejipanga kuhakikisha bodi hiyo inasonga mbele.

"Namshukuru Rais kwa kuniteua hivyo namwahidi nitafanya kazi vizuri ili kuendeleza Bodi ya Parole vizuri," alisema Mrema.

Kwa upande wa Kamishna Jenerali Suleiman Mzee ambaye ni Katibu wa Parole, alisema Sheria ya Bodi ya Parole iliyorekebishwa inazipa bodi ya taifa mamlaka ya kitaifa na mikoa kuwa na madaraka ya kudumu na kutekeleza ahadi walizotoa.

Alisema kwenye kipindi cha awamu ya saba, wamefanikiwa kujadili wafungwa 6,237, walitoka ni 5,535, na waliokataliwa kwa sababu mbalimbali ni 702.

# Bonite Bottlers yazindua Kilimanjaro lita 18.9

**Na Mwandishi Wetu**

KAMPUNI ya Bonite Bottlers Ltd (BBL) ya Moshi, mkoani Kilimanjaro imezindua maji ya Kilimanjaro katika ujazo mkubwa wa lita sita, 12 na 18.9.

Mkuu wa Mauzo na Masoko, Christopher Loiruk, alisema jana kuwa, Bonite imewekeza katika mitambo ya kisasa ya uzalishaji maji wa ujazo mkubwa ili kuwezesha wateja kuyapata kwa matumizi ya nyumbani, ofisini na taasisi.

"Maji ya Kilimanjaro katika ujazo mkubwa yanapatikana kwenye depoti zetu zote zilizoko mikoani, kwenye maduka na wazalishaji wa jumla nchi nzima," alisema.

Pia Loiruk alisema maji ya Kilimanjaro yanapatikana katika ujazo wa nusu lita, lita moja na lita moja na nusu.

"Tunawashukuru wateja wetu wote wa maji ya Kilimanjaro kwa kuendelea kutuunga mkono kwa sababu maji ya Kilimanjaro ni ya kuaminika kila siku," alisema.



Mkuu wa Mkoa wa Arusha, Mrisho Gambo (pili kushoto), akipata maelekezo kutoka kwa Mkurugenzi wa Mamlaka ya Majisafi na Majitaka Arusha (AUWSA), Mhandisi Justine Mwangijomba, alipotembelea moja ya matangi ya maji katika mradi wa maji wa kwa Tom, unaozalisha lita 50,000 kwa saa, uliopo wilayani Karatu, Mkoa wa Arusha juzi. **PICHA: WOINDE SHIZZA**

# RC aagiza mtendaji akamatwe madai ya ubadhirifu

**Na Neema Sawaka, KAHAMA**

MKUU wa Mkoa wa Shinyanga, Zainab Telack, amemwagiza Mkuu wa Polisi wa Ushetu, kumsaka na kumtia mbaroni Ofisa Mtendaji wa Kata ya Idahina, Halmashauri ya Ushetu, Issack Madale, anayedaiwa kukusanya shilingi milioni nane na kutoweka nazo.

Alitoa agizo hilo katika uwasilishaji majibu ya menejimenti kuhusu hoja za Mkaguzi wa Nje za mwaka unaoishia Juni 30, 2019, iliyoibuliwa kutoka hoja za miaka ya nyuma kuanzia 2013 hadi 2017.

Ilidaiwa kuwa ofisa mtendaji huyo, alikusanya fedha hizo kutoka makusanyo ya mapato ya ndani katika Kata ya Idahina, lakini hakuziwasilisha badala yake akatoweka nazo.

"Nakuagiza OCD Ushetu, Ofisa Mtendaji Kata, huyu asakwe popote alipo akamatwe afikishwe vyombo vya sheria, haiwezekani afanye uhalifu kisha aendelee kuwa huru uraiani," alisema Telack.

Mkurugenzi Mtendaji wa Halmashauri ya Ushetu, Michael Matomora, alisema suala hilo walishalifungulia kesi kituo kikuu cha polisi cha Ushetu, tofauti na inavyoelezwa.

"Tayari tumeishafungua kesi na RB ya kumtia mbaroni mtuhumiwa tunayo, tunashukuru tu kwa msisitizo uliotolewa wa kumtia mbaroni ili hatua zaidi za kisheria zichukuliwe dhidi yake," alisema Matomora.

Matomora alisema, kipindi kinachoishia mwaka wa fedha wa Juni 30, 2019, mkaguzi wa nje aliibua hoja 84 katika halmashauri hiyo, kati ya hizo; 48 ni za miaka 2013/2014 na 2016/2017 na jumla ya hoja 51 zilijibiwa na kufungwa.

Alisema hoja hizo ni sawa na asilimia 61, zilizobaki ziko katika hatua nzuri ya utekelezaji, huku akibainisha kuwa halmashauri hiyo kwa kipindi cha miaka mitatu mfululizo katika kaguzi za miaka ya fedha 2016/2017, 2017/2018 na 2018/2019, halmashauri hiyo imepata hatisafi.


## RIMINA AUCTION MART AND COMPANY LIMITED

### TANGAZO LA MNADA WA HADHARA

**Rimina Auction Mart** tutauza mali za wadaiwa za muda mrefu kama vitu vifuatavyo: Flat Body Trailer, Corporation Japan Chases No. KEFKE 600003071, Toyo Nyekundu Chases No. KEFKE 600002833 PLET No. T 450 CHA Colour Nyekundu T 734 AKG aina Fuso Mitsubish. T 599 ACH aina CANTER Mitsubish. T 372 BYL aina CARRY T 244 AMQ aina TOYOTA, Make Scania T 150 AZQ na vitu mbalimbali vya ndani katika Godown lililopo Majowe Kichangani Wilaya ya Ilala Mkoa wa Dar es salaam.

**MASHARTI YA MNADA**

- Mnada utafanyika mahali zilizopo mali zote tarehe 17/05/2020 siku ya Jumapili saa (4:00) nne asubuhi na kuendelea.

**Kwa maelezo zaidi wasiliana na Kampuni ya udalali ya Rimina Auction Mart jengo la Dewlo Kariakoo Mtaa wa Msimbazi/Rufiji Gorofa ya kwanza mkabala na DTB Bank. Simu namba 0763-375538 / 0715-385534 / 0716-686864.**

**WOTE MNAKARIBISHWA!**

157403

## BANI INVESTMENT LIMITED

### TANGAZO LA MNADA

KWA NIABA YA NMB MAKAO MAKUU, TUTAUZA KWA NJIA YA MNADA WA HADHARA MALI ZILIZOORODHESHWA HAPO CHINI AMBAZO ZILIWEKWA KAMA DHAMANA YA MKOPO. MNADA UTAFANYIKA MAHALI ZILIPO MALI HIZI SIKU NA SAA KAMA ILIVYOONYESHWA KATIKA JEDWALI LIFUATALO:

| Jina la Mdaiwa | Aina ya mali inayouzwa | Mahali ilipo | Tarehe ya Mnada | Muda wa Mnada |
|---|---|---|---|---|
| Hawte Investment Limited | Ware house prefabrication steel & sandwhich numbers in 3 No. 40ft containers on the site movement. | Mailikumi - Mtwara | 29.5.2020 &30.5.2020 | 4:00 asubuhi nakuendelea |
| Hawte Investment Limited | Shamba lililopo kwenye kiwanja na.1,Kitalu "A"CT Na. 11696 | Mailikumi - Mtwara | 29.5.2020 & 30.5.2020 | 4:00 asubuhi nakuendelea |
| Hawte Investment Limited | Shamba lililopo kwenye kiwanja na.2,Kitalu "A"CT Na. 11653 | Mailikumi - Mtwara | 29.5.2020 & 30.5.2020 | 4:00 asubuhi nakuendelea |
| Hawte Investment Limited | Shamba lililopo kwenye kiwanja na.3,Kitalu "A"CT Na. 11693 | Mailikumi - Mtwara | 29.5.2020 & 30.5.2020 | 4:00 asubuhi nakuendelea |
| Hawte Investment Limited | Shamba lililopo kwenye kiwanja na.4,Kitalu "A"CT Na. 11651 | Mailikumi- Mtwara | 29.5.2020 & 30.5.2020 | 4:00 asubuhi nakuendelea |
| ALBERT BENNIE CORNELIS | Nyumba iliyopo kwenye kiwanja no.46,Kitalu"B"Title no. 15178 | Ilemela-Mwanza | 30.5.2020 | 4:00 asubuhi |

**MASHARTI YA MNADA**

1. Mashamba/prefabrication steel & sandwhich zitauzwa "kama zilivyo " as where is basis"
2. Mnunuzi atakayeshinda atalipa malipo ya awali ya 25% ya bei ya mnada siku ya mnada na 75% katika muda wa siku 14
3. Mnunuzi atakayeshindwa kumalizia salio la 75% katika muda uliopangwa hapo juu hatarudishiwa fedha alizolipa awali na mnada utarudiwa siku nyingine itakayopangwa.
4. Gharama zote za kubadilisha hati miliki, kutwaa shamba/kumtoa mmiliki wa awali (ikiwa bado hajatoka hadi wakati wa mnada) na gharama nyinginezo zitakuwa juu ya mnunuzi.
5. Wateja wote mnakaribishwa kuona na kukagua shamba/container muda wote isipokuwa usiku.

**Kwa maelezo zaidi wasiliana na Ofisi ya:**
**BANI INVESTMENT LTD, S.L.P 71340 Dar es Salaam Lida Building, ghorofa ya 3 chumba No. 0313 Nkrumah Street.**
**Tel. 0713224578, 0677428873**

Nipashe
MWANGA WA JAMII

## Malalamiko unyanyapaa M'nyamala yachunguzwe

TUME ya Haki za Binadamu na Utawala Bora (THBUB), imeeleza kusikitishwa na taarifa ya vitendo vinavyofanywa na baadhi ya madaktari na wauguzi wa Hospitali ya Rufani ya Mkoa ya Mwananyamala jijini Dar es Salaam, vya kuwanyanyapaa na kuwasumbua wagonjwa wanaokwenda kupata matibabu.

Tume hiyo imesema wagonjwa hao wanatakiwa na hospitali hiyo kufanya vipimo vya virusi vya corona kabla ya kuanza kupata matibabu.

Taarifa ya Tume iliyotolewa na Mwenyekiti wake, Jaji mstaafu Mathew Pauwa Mhina Mwaimu, ilieleza kuwa wamesikitishwa na jambo hilo kwa sababu kila mwananchi ana haki ya kufurahia haki ya afya kwa kupata matibabu mazuri na ya uhakika.

Kwa mujibu wa Tume hiyo, madaktari na wauguzi wanapaswa kutambua kuwa sio kila mgonjwa ana maambukizo ya corona hivyo inaamini vitendo vya namna hiyo ni ukiukwaji wa haki ya afya kwa wananchi, na vinaweza kusababisha wagonjwa kupoteza maisha.

Kutokana na hali hiyo, Tume imeomba serikali iendelee kuhakikisha hospitali zinaendelea kutoa huduma nzuri kwa wagonjwa ili kuepusha malalamiko yasiyo ya lazima.

Aidha, Tume imeomba serikali kufanya uchunguzi wa kina ili kubaini chanzo cha vitendo hivyo vinavyofanywa na baadhi ya madaktari na wauguzi ili kuvitafutia ufumbuzi wa haraka.

Tunaamini kuwa THBUB imetoa taarifa hiyo kwa umma, baada ya kupokea malalamiko kutoka kwa umma sambamba na kufuatilia ili kujiridhisha kama yana ukweli ndani yake.

Sisi Nipashe tunaamini hivyo kwa kuwa chombo hicho kuwa huru, lakini kina ukaribu na serikali.

Aidha, Tume imeomba serikali kufanya uchunguzi wa kina ili kubaini chanzo cha vitendo hivyo vinavyofanywa na baadhi ya madaktari na wauguzi ili kuvitafutia ufumbuzi wa haraka.

Tunaamini kuwa Tume imetoa taarifa ya masikitiko yake hadharani baada ya kupokea malalamiko na kufuatilia kama yana ukweli ndani yake. Tunasema hivyo kwa kuwa chombo hicho kinaundwa na watu mahiri, wenye ujuzi na weledi katika tasnia mbalimbali hususan ya sheria.

Vile vile Tume hii inateuliwa na Rais wa Jamhuri ya Muungano wa Tanzania, hivyo inapotoa tamko, inamaanisha kuwa imelifanyia uchambuzi wa kutosha kabla.

Malalamiko ya watu wanaokwenda kupata huduma katika vituo vya huduma hususan kipindi hiki cha ugonjwa wa Covid-19 kuhusiana na kuzungushwa katika kupatiwa huduma ni mengi, hivyo tunaona kuwa sasa ni wakati mwafaka kwa serikali kutafanyia uchunguzi.

Kama kuna watoa huduma wakiwamo madaktari na wauguzi wanaoendelea kufanya unyanyapaa dhidi ya wagonjwa wachukuliwe hatua za kisheria na za kinishamu kutokana na kuwanyima watu haki yao ya msingi ya kupata huduma za afya.

Tunapendekeza hatua hizo kwa kuwa Waziri wa Afya, Ummy Mwalimu, hivi karibuni aliwaonya watoa huduma za afya, alipotembelea Hospitali ya Mwananyamala na kufuatia malalamiko hayo.


Pengine ndiyo maana hata THBUB imempongeza Waziri Mwalimu, kwa kuchukua hatua za haraka za kukemea vitendo hivyo vya baadhi ya madaktari na wauguzi, ambavyo vinaweza kuchafua taswira nzuri ya sekta ya afya na jitihada mbalimbali zinazochukuliwa na serikali.

Vituo vya huduma zikiwamo hospitali zinapaswa kuwa mahali rafiki kwa wagonjwa ili mtu anayehitaji matibabu aone kuwa ndipo mahali salama kwake kuokoa maisha yake.

Kinyume chake, wagonjwa hawawezi kukimbilia huko kwa kuwa ni mahali hatari kwa usalama wa maisha yao. Ikumbukwe kuwa kunyanyapaa wagonjwa na kuwasababishia kukosa huduma za afya ambazo ni haki ya msingi kwa wakati mwafaka, kunaweza kusababisha athari kubwa, vikiwamo vifo.

Nipashe hutolewa na kuchapishwa na:
**THE GUARDIAN LIMITED**

**Mhariri Mtendaji :** Beatrice Bandawe
**Mneja Usambazaji na Masoko:** Emmanuel Lyimo, 0716 500500
**Mapokezi:** 0745 700710
**Matangazo:** 0782253676
Baruapepe: advertise@guardian.co.tz
**Website:** www.ippmedia.com
epaper.ippmedia.com




## Muungwana Lazima Nilonge



# Ushirika unapokiuka malengo yake, kudumu ni kitendawili

Na Sabato Kasika

**KATIKA** harakati za kujikomboa kiuchumi, vyama vya ushirika vimekuwa na mchango mkubwa kutetea hali ya uchumi kwa wanachama na wanajamii kwa ujumla.

Hilo limo katika majukumu muhimu yanayofanywa na vyama hivyo vya ushirika katika kupunguza umaskini na kukuza huduma za kiuchumi, kibiashara na masoko kwa wakulima wadogo.

Vilevile, inawapa sauti wadau wanyonge, kuwaletea ustawi wa jamii, kutengeneza ajira, kurahisisha upatikanaji huduma za kifedha na kuwezesha wakulima na jamii kwa ujumla.

Aidha, vyama hivyo ambavyo ni nguzo muhimu katika jamii, vina mchango mkubwa katika kuinua hali za kiuchumi za wanachama, kuwaunganisha wananchi wa hali ya chini, ili waweze kujitambua na kuunganisha nguvu zao katika kujiletea maendeleo.

Pia, vyama vya ushirika vinatajwa kuwa na uwezo wa kuwaunganisha wanyonge, ili waweze kutetea haki zao na kuwapa uwezo wa kujadiliana na kupambana na walanguzi ili kupata bei bora ya mazao yao.

Hata hivyo, kuna baadhi ya vyama hivyo vimekuwa vikikabiliwa na changamoto mbalimbali zikiwamo zinazosababisha na viongozi na kusababisha wanachama kuvikimbia.

Miongoni mwa changamoto zilizopo ni tabia ya uendeshaji wa vyama hivyo, bila ya kufuata taratibu na kuna wakati wakulima ambao ni wanachama walidhulumiwa fedha za mauzo ya zao yao, kupitia vyama vyao.

Ni hivi karibuni, Waziri wa Kilimo, Japhet Hasunga, aliainika katika faragha yake na Nipashe kwamba, Ripoti ya Ukaguzi wa Vyama vya Ushirika ya Mwaka 2018/2019 kwa Kamishna Mkuu wa Taasisi ya Kuzuia na Kupamba na Rushwa (Takukuru), Brigedia Jenerali John Mbung'o, ilikuwa na 'madudu' mengi.

Ukaguzi huo ulibaini ubadhirifu wa zaidi ya Sh. bilioni 124.5 uliofanywa na vyama vikuu vya ushirikia vya akiba na mikopo maarufu 'saccos' na vyama vya msingi vya mazao vinavyojulikana kama 'amcos.'

Kupitia taarifa hiyo, ilibaini kuwapo vyama vya ushirika vilivyokiuka misingi ya uendeshaji na vikaumbuka na yaliyo kinyume na misingi ya kisheria na kanuni za uendeshaji ushirika nchini.

Ni siku kadhaa zilizopita, Waziri Hasunga alitangaza kufuta usajili wa vyama vya ushirika 3, 348 vilivyokuwapo rasmi kisheria, baada ya kupatiwa notisi ya kusudio hilo, sababu kuu inatajwa vilikuwa havitekelezi majukumu yake ya msingi kwa mujibu wa usajili uliotolewa na Mrajis wa Vyama vya Ushirika nchini.

Kuna msemo wa Kiswahili 'ukiona mwenzio ananyolewa na wewe tia maji.' Binafsi nasema, hilo linapaswa kuwa fundisho kwa vyama vingine vya ushirika vilivyobaki, vibaki katika mstari wa kisheria, katika uendesha shughuli zake kwa namna inavyotakiwa.

Ikumbukwe kwamba waziri huyo mwenye dhamana, ameshaweka wazi kwamba, hatua ya kuvifuta vyama vinavyokiuka misingi na kanuni za usajili wake, utakuwa endelevu dhidi ya vyama vya ushirika vitakavyoshindwa kutekeleza malengo ya uanzishwa wake, kwa mujibu wa Sheria ya Vyama vya Ushirika iliyopo.

Kinachosisitizwa na waziri, ni uadilifu katika utendaji ili vyama vya ushirika viendelee kuwa nguzo imara ya kuwakomboa wananchi kutoka kwenye umaskini, kwani vina mchango mkubwa katika kuboresha maendeleo ya nchi.

Iwapo vyama vya ushirika wa mazao, akiba na mikopo na aina nyingine vitajiendesha vizuri, kuna uhakika wa kutoa ajira kwa wanachama wake na ndio ngazi mojawapo muhimu ya kupiga hatua kimaendeleo.

Hivyo suala la kujiendesha kwa kuzingatia misingi ya uanzishaji wake ni njia ambayo kwa namna moja au nyingine inaweza kusaidia vyama kutimiza hayo na vikaaminika kwa wanachama.

Hapa sibahatishi kutumia mfano wa Chama cha Ushirika cha Umoja, kilichopo mjini Liwale mkoani Lindi, kwa kufanikiwa kuwasomesha wanachama wake na waliopata utaalamu wa mambo ya fedha na kisha wakawaajiri.

Ni hatua nzuri, kwani badala ya kuajiri wataalamu kutoka nje, kikaona umuhimu wa kuwaendeleza wanachama wake na kisha kutumikia kuiweka sawa hesabu zao za fedha, wakiwa ni wataalamu wa ndani waliiopiga hatua za ujuzi na maarifa.



Mkuu wa Mkoa wa Mwanza, John Mongella (katikati), akipokea moja ya vidumu vya vitakasa mikono (Sanitizer) kutoka kwa Meneja wa kiwanda cha bia cha TBL, tawi la Mwanza, Patel Kilovele, jana. TBL imetoa lita 500 za sanitizer ili kupambana na maambukizo ya Covid-19. Kulia ni Katibu Tawala wa mkoa huo, Emmanuel Tutuba.
**PICHA: MPIGAPICHA WETU**

# Wacharuka wafugaji kupokwa mifugo yao

**Na Gwamaka Alipipi, DODOMA**

WABUNGE wameibana serikali wakiitaka kutatua tatizo la baadhi ya askari wa wanyamapori kuwanyang'anya wafugaji mifugo yao.

Wakichangia mjadala wa makadirio ya mapato na matumizi ya Wizara ya Mifugo na Uvuvi kwa mwaka ujao wa fedha, wabunge hao walisema askari wa wanyamapori wamekuwa wakikamata mifugo ya wafugaji na kuwadhulumu pindi mifugo inapoingia katika hifadhi.

Mbunge wa Simanjiro (CCM), James Ole Millya, aliitaka serikali kushughulikia matatizo ya wafugaji kwa kuwa wengi wao wamekuwa wakinyang'anywa mifugo yao na askari wa wanyamapori.

Alisema hata inapotokea wafugaji wanarudishiwa mifugo yao pindi wanaposhinda kesi, hupewa mifugo pungufu kulinganisha na idadi kamili iliyokamatwa.

Millya alisema kumekuwa na uonevu mkubwa wa uporaji wa mifugo, akibainisha kuwa mfugaji anaporwa mifugo 300, lakini baada ya miaka mitatu unamrudishiwa ng'ombe 100.

Mbunge wa Mbinga Mjini (CCM), Sixtus Mapunda, aliipongeza wizara hiyo kwa kutatua migogoro ya wakulima na wafugaji nchini, huku akitaka uwekwe utaratibu wa kuwatengea maeneo wafugaji ili waache tabia ya kuingiza mifugo katika mbunga za wanyama.

"Wafugaji hawana shida wanaingia katika maeneo katika kipindi ambacho hakuna nyasi, lakini ng'ombe anakula nyasi, hali miti kwanini, tusitengeneze utaratibu maalum wa kuingia ng'ombe kwani wataleta mbolea?" Mapunda alihoji.

Hata hivyo, tayari ilishaelezwa na wataalamu wa masuala ya uhifadhi kuwa mwingiliano wa mifugo na wanyamapori ni hatari kwa kuwa husababisha kuenea kwa magonjwa ya wanyamapori kwenda kwa mifugo na kinyume chake.

Mbunge wa Viti Maalum (CCM), Martha Umbulla, alisema jamii ya wafugaji imekuwa na malalamiko mengi ambayo yanatakiwa kusikilizwa na kutatuliwa.

Umbulla alisema: "Kilio hicho siyo cha leo, mimi ninatoka katika jamii ya wafugaji, malalamiko haya ni ya kweli, ifike mahali yaangaliwe. Kwa kufanya hivyo, tutaweka utulifu katika ufugaji. Wafugaji wanamshukuru Rais kutokaka na kuunda timu ya kutatua migogoro lakini ni lazima itatuliwe kwa wakati," alisema.

Wabunge wengine waliochangia hoja hiyo ni wafugaji kuonewa ni Mbunge wa Kondoa Mjini, Edwin Sannda (CCM), na Mbunge wa Monduli (CCM), Julius Kalanga.

**MAJIBU YA SERIKALI**

Mwanasheria Mkuu wa Serikali (AG), Prof. Adelardus Kilangi, akichangia mjadala huo, alisema ukamataji wa mifugo unafanyika kwa mujibu wa sheria ambayo ilitungwa na wabunge wenyewe.

Alisema utekelezaji wa sheria hiyo unakumbana na vikwazo kadhaa, lakini serikali inaendelea kutatua matatizo yanayojitokeza.

Alisema mahakama inapotoa hukumu na mifugo kuendelea kushikiliwa, kunaweza kuwa na tatizo sehemu fulani, hivyo serikali itafuatilia kwenye kesi zote ili kufahamu ni kesi gani ambazo zimeshatolewa hukumu, lakini mifugo bado inaendelea kushikiliwa.

Kuhusu Mkurugenzi wa Mashtaka (DPP) kukata rufani pindi mfugaji anaposhinda kesi, Prof. Kilangi alisema: "Majukumu ya DPP yapo kikatiba na hayaingiliwi na mtu yeyote. Anapokata rufani, anakuwa na sababu ya kufanya hivyo, inawezekana kuna kutafsiriwa vibaya kwa sheria."

# Matatani madai uhusiano kimapenzi na mwanafunzi

**Na Said Hamdani, LINDI**

JESHI la Polisi wilayani Lindi, inamshikilia mfanyabiashara wa kuuza nafaka katika Manispaa ya Lindi, Evon Sanga, mkazi wa kata ya Nachingwea, kwa madai ya kuwa na mahusiano ya kimapenzi na mwanafunzi.

Mtuhumiwa anadaiwa kuwa na mahusiano hayo na mwanafunzi wa kidato cha nne katika Shule ya Sekondari Angaza.

Kamanda wa Polisi mkoani Lindi, Stanley Kulyamo, alisema kuwa mtuhumiwa huyo alikamatwa Mei 11, mwaka huu, saa 5:00 usiku katika nyumba ya kulala wageni Kata ya Mikumbi.

Akielezea tukio hilo, Kamanda huyo alisema kukamatwa kwa mfanyabiashara huyo kumetokana na ushirikiano kati ya mzazi na polisi, kufuatia binti yao kuonyesha mabadiliko ya kitabia ikiwamo ya kutoonekana nyumbani.

Kwa mujibu wa Kamanda Kulyamo, kutokana na mabadiliko hayo mzazi wa mwanafunzi huyo Aprili 23, mwaka huu, aliripoti kituo cha polisi kuwa amepokwa binti yake.

"Baada ya Aprili 21 mwaka huu, binti yake haonekani nyumbani kwao, Aprili 23, mwaka huu, alikwenda kituo cha polisi kutoa taarifa ya kupokwa kwa binti yake," alisema kamanda.

Alisema Mei 11, mwaka huu, usiku wa saa 5:0, askari wakiwa wanatekeleza majukumu yao ya kikazi walimkamata kufika nyumba ya wageni na kumkuta mtuhumiwa akiwa na mwanafunzi huyo.

Kamanda Kulyamo alisema uchunguzi wa awali umebaini kuwa Jeshi hilo, wamebaini mwanafunzi huyo amepangiwa kuishi chumba hicho tangu Aprili 10, mwaka huu.

Alisema mtuhumiwa atafikishwa mahakamani muda wowote baada ya upelelezi kukamilika.

**"Baada ya Aprili 21 mwaka huu, binti yake haonekani nyumbani kwao, Aprili 23, mwaka huu, alikwenda kituo cha polisi kutoa taarifa ya kupokwa kwa binti yake," alisema kamanda.**

**GSP AUCTION MART**

**KUMB No. TATA/2020/DM/005**

GSP AUCTION MART Kwa idhini na mamlaka tuliyopewa na kampuni ya ALLIANCE FINANCE CORPORATION LIMITED S.L.P 40780 Dar es salaam tunapenda kutangaza mnada wa hadhara wa kuuza Magari kwa njia ya mnada wa magari twaja hapo chini. Siku ya ijumaa tarehe 29/05/2020 mnada utaanza Saa 5:00 kamili asubuhi katika yadi ya ALLIANCE FINANCE CORPORATION LIMITED iliyopo Dar es salaam vingunguti , Arusha na Mwanza.

| | | | |
|---|---|---|---|
| JAMES ANTHONY MMASSY | LP 909 | T432 DPS | DAR-ES-SALAAM |
| LUSUBILO JOSEPH KAJANGE | LPK 813 | T791 DRD | MWANZA |
| MAJID AHMED IDD | Ultra Bus | T773 DQM | MWANZA |
| MAJID AHMED IDD | Ultra Bus | T613 DQF | MWANZA |
| TWAHIL ABDALLAH MPULUJI | LPO 10.2T/52 | T167 DPU | DAR-ES-SALAAM |
| CONSTANTINO MLAGALA MSONJELA | LP 909 | T881 DNQ | MWANZA |
| CONSTANTINO MLAGALA MSONJELA | LP 909 | T487 DNR | DAR-ES-SALAAM |
| ELIAS DEBLO ELIA | LPO 10.2T/52 | T906 DPK | DAR-ES-SALAAM |
| JUED HOMES LTD | LP909 Bus | T517 DNS | DAR-ES-SALAAM |
| JUED HOMES LTD | LP909 Bus | T207 DNS | DAR-ES-SALAAM |
| JUED HOMES LTD | LP909 Bus | T722 DNQ | MWANZA |
| JUED HOMES LTD | LP909 Bus | T814 DMQ | DAR-ES-SALAAM |
| RICHARD PAUL CHAMA | LP909 Bus | T452 DNW | MWANZA |
| VINCENT CHIMI MASANJA | LPO 10.2T/52 | T387 DPZ | MWANZA |
| MRIDU HAMADI MTOO | LPO 10.2T/52 | T866 DRG | ARUSHA |
| THEOBALD NICAS MPIRI | LP909 Bus | T996 DPL | DAR-ES-SALAAM |
| THEOBALD NICAS MPIRI | LP909 Bus | T681 DPM | DAR-ES-SALAAM |
| SALVANUS JOHN CHIDOWE | LP909 Bus | T870 DPA | DAR-ES-SALAAM |

1. Dhamana itauzwa kama ilivyo.
2. Mnunuzi anatakiwa kulipa siku hiyo hiyo ya mnada asilimia 25% ya bei iliyofikiwa.
3. Malipo ya asilimia 75% yalipwe ndani ya siku kumi na nne (14) kukamilisha malipo yote ukishindwa kufanya hivyo mnunuzi atakuwa amepoteza malipo yote ya awali ya asilimia 25% na mnada utarudiwa tena.
4. Gharama za kuona, kukaguwa, kuhamisha umiliki ni juu ya mnunuzi.
5. Kwa yeyote atakayeharibu mnada hatua kali za kisheria zitachukuliwa dhidi yake.

**KWA TAARIFA ZAIDI WASILIANA NA:**
**GSP AUCTION MART PO BOX 310088 DAE ES SALAAM.**
**+255 654 922 892, +255 687 638 679**

# Asasi kuzindua mradi kudhibiti Covid-19

**Na Happy Severine, ITILIMA**

ASASI ya Kawiye Development, imezindua mradi wa kudhibiti ugonjwa wa Covid-19 katika Wilaya ya Itilima mkoani Simiyu ambao utawafikia wananchi 60,000.

Mradi huo umelenga zaidi kuwajengea uwezo wanawake, wazee na watoto kujikinga na maradhi hayo kutokana na kuwa kwenye hatari kubwa ya kuambukizwa.

Akizungumza wakati wa uzinduzi huo jana, Mkurugenzi wa asasi hiyo, Ezekiel Kasanga, alisema utekelezaji wa mradi utahusisha viongozi wa serikali ngazi ya wilaya, idara ya afya, wenyeviti wa vijiji, viongozi wa dini, waganga wa tiba asili na wahudumu wa afya ngazi ya jamii (CHWs).

"Tunatarajia kuwafikia wananchi 60,000 na hatimaye kuimarisha uelewa na uwezo wa wana jamii kudhibiti maambukizo na madhara ya ugonjwa wa Covid-19 wilayani Itilima," alisema Kasanga.

Alisema mradi huo, utagharimu Sh. 30,000,000 ambazo ni ruzuku kutoka Shirika la Kizalendo la Foundation for Civil Society (FCS).

# Bavicha yamtaka Spika Ndugai kuheshimu uamuzi wa chama

**Na Elizabeth Zaya**

MWENYEKITI wa Taifa wa Baraza la Vijana la Chama cha Demokrasia na Maendeleo (Bavicha), John Pambalu, amemtaka Spika wa Bunge, Job Ndugai, kuheshimu uamuzi wa chama hicho wa kuwavua uanachama wabunge wake wanne.

Pambalu alisema ni vema Spika akafahamu kwamba uamuzi wa kuwafukuza uanachama wabunge hao haukufanywa na Mwenyekiti wa Chadema peke yake kama anavyodai yeye.

"Tunamtaka Spika kuheshimu uamuzi wa Kamati Kuu ya Chadema wa kuwavua uanachama wabunge wake wanne. Kama kuna mtu aliyemdanganya kwamba uamuzi huo ulifanywa na mwenyekiti peke yake, kamdanganya kweli kweli," alisema Pambalu.

"Na kama hasikilizi tutampelekea video tulizofanya mkutano kwa njia ya kidigitali ili aone vizuri maazimio yaliyofanywa katika mkutano wa Kamati Kuu na mimi nikiwa miongoni mwa walioshiriki mkutano huo kama mwakilishi wa vijana," anaongeza.

Alisema Spika kushindwa kuheshimu uamuzi wa Kamati Kuu ya Chadema ni kwenda kinyume cha Katiba ya Jamhuri ya Muungano wa Tanzania.

"Spika anapaswa aheshimu mawazo ya chama chetu na aiheshimu, ailinde na aitetee Katiba ya Jamhuri ya Muungano wa Tanzania kwa sababu ndiyo msingi wa kila kitu kwa sasa. Katiba iko wazi kabisa na inasema kwamba mtu atapopoteza sifa zake za kuwa mbunge pindi atakapokosa kuaminiwa na chama chake kilichompa ridhaa ya nafasi yake hiyo," alisema Pambalu.

"Huyu Spika anashangaza sana, juzi hapa amemrudisha bungeni aliyekuwa Mbunge wa Ndanda, Cecil Mwambe, ambaye tayari alikuwa amejiondoa mwenyewe kwenye chama cha Chadema kwa kutangaza hadharani, badala ya kuangalia Katiba inasema nini kwa mtu wa namna hiyo yeye anamrudisha bungeni."

"Kama hiyo haitoshi wabunge ambao wamevuliwa uanachama anatangaza kwamba eti bado anawatambua," alisema.

Alisema ni vema Ndugai akakumbuka namna alivyowahi kuheshimu matakwa ya kikatiba kwa kuheshimu uamuzi uliowahi kufanywa na Chama cha Wananchi (CUF) wa kuwavua uanachama wabunge wake wa viti maalum, uliofanywa na Mwenyekiti, Prof. Ibrahim Lipumba.

"Nimkumbushe Spika kwamba kipindi kile kilipowafukuza uanachama wabunge wake na baada ya kupelekewa barua aliheshimu ule uamuzi, tunamuomba aheshimu vile vile uamuzi wa Chadema na Katiba ya Jamhuri," alisisitiza Pambalu.

Wabunge waliovuliwa uanachama na Chadema ni Wilfred Lwakatare (Bukoba Mjini), Antony Komu (Moshi Vijijini), David Silinde (Momba) na Joseph Selasini (Rombo).



Mwenyekiti wa Baraza la Vijana la Chama cha Demokrasia na Maendeleo (Chadema), Jimbo la Shinyanga Mjini, Samson Ngw'agi (kulia), akizungumza na waandishi wa habari, jimboni humo jana, akimtaka Spika Job Ndugai, kuwafukuza Bungeni wabunge wanne waliofukuzwa na chama hicho, kwa madai hawana sifa tena ya kuwa wabunge. Kushoto ni Katibu wa Baraza hilo, Alfred Masanja. **PICHA: MARCO MADUHU**

# Mbaroni kujifanya maofisa NEMC

**Na Rose Jacob, MWANZA**

BARAZA la Taifa la Hifadhi na Usimamizi wa Mazingira (NEMC), linawashikilia watu watatu kwa tuhuma za kujifanya maofisa wa baraza hilo na kutapeli wawekezaji kwa kujipatia kazi ya tathmini ya athari za mazingira.

Pia, wamedaiwa kupeleka taarifa za miradi kwenye baraza kwa ajili ya usajili, kwa kutumia majina ya wataalamu waliosajiliwa, jambo lililolifanya baraza kutojua kama sio halali.

Akizungumza ofisini kwake, Kaimu Meneja wa NEMC, Mhandisi Redempta Samwel, alisema, matapeli hao wamekuwa wakipita maeneo mbalimbali ya Kanda ya Ziwa na kushindwa kuwafikishia wawekezaji barua zinazotoka baraza na hivyo wengi wao kushindwa kupata cheti cha mazingira.

"NEMC Kanda ya Ziwa kwa kushirikiana na vyombo vya ulinzi na usalama tumefanikiwa kuwakamata watuhumiwa watatu ambao, wamekuwa wakijitambulisha kwa wawekezaji kuwa wao ni maofisa wa NEMC hivyo wanafanya tathmini ya athari ya mazingira na ukaguzi," alisema Redempta.

Akithibitisha kukamatwa kwa watuhumiwa hao, Kamishna Msaidizi wa Jeshi la Polisi mkoani Mwanza, Safia Jongo, alisema watuhumiwa Hafashimana Jacob (47), Gibson Kabamba (36) na Thobias Kabadi (43), wanawashikilia kwa makosa ya kujifanya maofisa wa NEMC.

"Ni kweli tunawashikilia watuhumiwa hao ambao mbali na kujifanya maofisa wa NEMC, wamekuwa wanajifanya wawekezaji na kumtafuta mtaalamu mshauri na kuingia naye mkataba na baadaye kukwamisha mchakato kwa kutelekeza miradi," alisema Jongo.

Jongo alisema uchunguzi ukikamilika watawafikisha mahakamani watuhumiwa hao kwa mujibu wa sheria.

# Mwili wa mtoto waopolewa ndani ya dimbwi

**Na Restuta Damian, BUKOBA**

JESHI la Zimamoto na Uokoaji mkoani Kagera limeopoa mwili wa mtoto mwenye umri wa mwaka mmoja katika dimbwi la maji yaliyotuama kwa mvua, Mtaa wa Nyamkazi, Manispaa ya Bukoba, mkoani Kagera.

Mkuu wa jeshi hilo mkoani hapo Inspekta Hamis Dawa, alisema majira ya 12:58 jioni juzi alipokea taarifa kuhusu tukio hilo.

Dawa alisema taarifa za awali zilieleza kuwa mtoto huyo alitoweka nyumbani kwa muda mrefu.

"Kwa taarifa za awali ni kwamba mtoto huyo alitoweka nyumbani, muda ulivyoenda zaidi ndipo walianza kutafuta ikiwa ni siku nzima ndipo walibaini akiwa amefariki ndani ya maji ya dimbwi," alisema Dawa.

Alisema mama wa marehemu, Disela Mwombeki, alitoka nyumbani kwake kumtafuta mwanawe baada ya kubaini hajaonekana nyumbani kwa muda mrefu.

Kamanda huyo alisema hilo ni tukio la pili la kuopoa mtoto kwenye mto na madimbwi ya maji katika kipindi hiki cha mvua.

# Mwanakijiji afa kwa kuliwa na simba

**Na Neema Hussein, KATAVI**

MKAZI wa Manispaa ya Mpanda mkoani Katavi, Songambele Alikado (68), amekufa baada ya kuliwa na simba.

Tukio hilo limetokea katika Kijiji Cha Stalike, wakati Songambele akielekea nyumbani kwake maeneo ya mashambani Kabanga.

Jeshi la Polisi limethibitisha kutokea kwa tukio hilo jana, ambapo Kamanda wa Mkoa wa Katavi, Benjamin Kuzaga, alisema Songambele alikuwa anaelekea nyumbani kwake Kabanga Stalike karibu na Hifadhi ya Taifa Katavi.

Alisema Mwenyekiti wa Kijiji cha Stalike, Seleman Ramadhan, aligundua kuwa mwananchi wake kaliwa na simba ndipo alipotoa taarifa kwa Jeshi la Polisi.

Kuzaga alisema mwili wa Songambele baada ya kufanyiwa uchunguzi na madaktari, ulikutwa umeliwa mguu mmoja wa kulia na sehemu zake za siri, na kwamba mwili huo umeshakabidhiwa kwa ndugu, kwa ajili ya maziko.

Kutokana na tukio hilo, Jeshi la Polisi limewataka wananchi kuchukua tahadhari dhidi ya wanyama wakali kwa kutoa taarifa wanapoonekana katika makazi ya watu.



Abiria wakiingia katika daladala kwenye kituo cha Mbezi Mwisho, jijini Dar es Salaam jana, katika mazingira ya kusongamana, ambayo ni hatari kwa maambukizo ya virusi vya corona. **PICHA: SABATO KASIKA**

## Wilaya Ikungi yakarabati shule zake

**Na Elisante John, SINGIDA**

HALMASHAURI ya Ikungi, mkoani Singida, imetumia muda wa shule kufungwa kwa sababu ya corona, kukarabati miundombinu ya shule za msingi kwa ushirikiano na jamii chini ya mpango wa Equip Tanzania.

Akizungumza na Nipashe, Mkurugenzi Mtendaji wa halmashauri hiyo, Justice Kijazi, alisema maboresho hayo yanalenga kuhakikisha wanafunzi wanasoma katika mazingira mazuri.

Alisema mpango huo ulioanza mwaka 2018 kwa ajili ya kuinua ubora wa elimu, na kwamba umeweza kufanikisha ujenzi wa vyumba vinane vya madarasa, matundu 24 ya vyoo, ofisi nne za walimu na mafunzo kwa walimu na wazazi.

"Tumejenga maboma ya vyumba sita vya maabara kwa takribani Sh. milioni 74.4, Sh. milioni 84 tumepeleka kwenye shule zetu 108, kwa takribani kila shule imepata Sh. 400,000...zaidi ya watu 650 wamepatiwa mafunzo mbalimbali kuimarisha umoja baina ya walimu na wazazi," alisema.

Aidha, Kijazi aliitaka jamii kuendelea kushirikiana na halmashauri hiyo, ili kuwezesha mpango wa kuinua ubora wa elimu wilayani Ikungi kupitia Equip-Tanzania, uzae matokea bora kwa ajili ya watoto wao.

Naye, Mratibu wa Equip-Tanzania Wilaya ya Ikungi, Imani Maketa, alisema kuwa kupitia mpango huo kwa sasa jamii imefanikiwa kusimamia vema shule zake zote, na hivyo taaluma kuweza kuimarika zaidi katika wilaya hiyo.

"Jamii imepatiwa sana mafunzo na hivyo imekabidhiwa kama mali yao, hivi sasa wamekuwa na uelewa zaidi wa namna ya kuziendesha... baada ya kupatiwa mafunzo wamekuwa wasimamizi wazuri na waaminifu wakubwa, kwa kushirikiana pia na kamati na walimu," alifafanua Maketa.

Ikungi ina jumla ya shule za msingi 108, na hadi kufikia Aprili mwaka huu, Equip-Tanzania ilitumia zaidi ya Sh. bilioni 1.1, kuimarisha sekta ya elimu ya msingi.

**"Tumejenga maboma ya vyumba sita vya maabara kwa takribani Sh. milioni 74.4, Sh. milioni 84 tumepeleka kwenye shule zetu 108, kwa takribani kila shule imepata Sh. 400,000... zaidi ya watu 650 wamepatiwa mafunzo mbalimbali kuimarisha umoja baina ya walimu na wazazi," alisema.**

## Wakunwa upatikanaji gari la wagonjwa

**Restuta Damian, BUKOBA**

BAADHI ya wakazi wa Kijiji cha Bushagara na Rushaka Kata ya Buhendangabo Wilaya ya Bukoba mkoani Kagera pamoja na wauguzi wa Zahanati ya Kalema, wameushukuru uongozi wa kata kufanikisha kupatikana kwa gari la kubebea wagonjwa wa dharura (ambulance).

Kukosekana kwa gari hilo ilikuwa changamoto kubwa kwa wakazi hao, hivyo kuushukuru uongozi wa kata kupitia kwa Diwani Audax Kaijage, kufanikisha upatikanaji wake.

Wakizungumza kwa nyakati tofauti baada ya kupokea gari hilo ambalo litatoa huduma ya wagonjwa wa dharura panapotokea tatizo katika zahanati hiyo yenye kuhudumia wakazi wa vijiji vya Rushaka, Kibale, na Bushagara.

Prospa John, mkazi wa Bushagara, alisema, gari hilo limekuja kwa wakati ambao kuna ugonjwa wa virusi vya corona, na kwamba litasaidia kwa kurahisisha huduma za kubeba washukiwa wenye dalili zinazotajwa na wataalamu.

Alisema mbali na ugonjwa huo, wananchi walipata changamoto ya kupata usafiri wa kuwapeleka kwenye rufani baada ya kuwa imeshindikana kutibiwa katika zahanati hiyo na kuingia gharama za kukodi pikipiki au teksi.

"Hapa ni furaha ya kupunguziwa gharama kwani ilikuwa inagharimu sana mfano, una mzazi anatozwa shilingi 50,000/100,000 kumfikisha hospitali aliyopangiwa iwe usiku au mchana," alisema John.

Retisia Jovin, mkazi wa kijiji cha Rushaka, alisema kulikuwa na uhitaji mkubwa kwa wajawazito, ambao wengi wao ndio wanaopewa rufani kwenda Hospitali ya Mkoa ambako ni mbali.

Alisema awali zahanati ilikuwa inatumia gari kutoka Kata ya Nyakato ambayo ni jirani, lakini lilikuwa linachelewa na kuwalazimu kuchukua usafiri wa kawaida ili kuwahi huduma.

"Kama unavyojua vya kuazima, ilikuwa inachelewa au imepeleka mgonjwa kwanza wa zahanati nyingine ndipo ikufuate," alisema na kuongeza:

"Kwa kipindi hiki tunaamini kutakuwa na badiliko kubwa na huduma hiyo kwetu sisi kinamama na wagonjwa."

Diwani wa Kata ya Butelangabo, Kaijage, alisema sababu ya kutafuta huduma ya gari ni kuwapo na matukio ya radi nyakati za mvua mara kwa mara katani hapo.

Kaijage alisema, upatikanaji ni juhudi za halmashauri kuchangisha fedha za kununua, baada ya kuona suala hilo likiingizwa katika mizunguko ya serikali itachelewesha wananchi, hivyo ombi lilipelekwa na kwenye uongozi wa halmashauri wilaya hiyo.

Kwa upande wake Tabibu Msaidizi katika Zahanati hiyo, Dismas Dominick, alisema, zahanati hiyo hutoa huduma mbalimbali na kufikia wagonjwa 350 hadi 400 kwa mwezi.

Alisema licha ya changamoto ya miundombinu ya maji, nishati ya umeme wa uhakika, vifaa vya maabara na ufinyu wa bajeti ya dawa, bado wananchi 4,847 wanaitegemea zahanati hiyo.

Naye Mganga Mkuu wa Wilaya hiyo, Bantioti Gabriel, alisema wilaya hiyo ina vituo vya afya 36 zahanati zaidi 40 zenye magari ya wagonjwa matatu yaliyogawanywa kwa kuangalia uhitaji.

Hata hivyo alisema ongezeko la gari lilitolewa na Diwani wa Kata hiyo litapunguza uhitaji.

# Serikali yafafanua utaratibu wa matumizi ya silaha kwa wamiliki

Na Augusta Njoji, DODOMA

BUNGE limeelezwa kuwa silaha itatumiwa na mmiliki wakati wowote kwa matumizi halali yanayozingatia matakwa ya sheria.

Hata hivyo, matumizi ya silaha yanayosababisha kifo hayakubaliki kisheria kwa kuwa mmiliki wa silaha anao wajibu wa kutumia silaha kwa usahihi bila kuleta madhara kwa wengine.

Utafanuzi kuhusu utaratibu wa matumizi ya silaha ulitolewa bungeni jana na Wizara ya Mambo ya Ndani ya Nchi wakati ikijibu swali la Mbunge wa Konde (CUF), Khatibu Saidi Haji.

Katika swali lake, mbunge huyo alisema serikali hutoa vibali vya kumiliki silaha kisheria kwa raia wake kwa ajili ya kujilinda.

"Je, ni wakati gani na matukio gani ya hatari ambayo mmiliki wa silaha anapotumia silaha au hata kuua hatakuwa na hatia?" Alihoji.

Katika majibu ya wizara hiyo, ilisema mmiliki wa silaha anaweza kuitumia silaha yake katika hali ya kujihami yeye mwenyewe, kumhami mtu mwingine ama mali dhidi ya hatari au tukio ambalo linaweza kuleta madhara makubwa dhidi ya maisha au mali.

"Matumizi ya silaha yanayosababisha kifo hayakubariki kisheria kwani mmiliki wa silaha anao wajibu wa kutumia silaha kwa usahihi bila kuleta madhara kwa wengine," ilisema.

Aidha, ilisema yapo mazingira ambayo mmiliki wa silaha wakati akijilinda ama kumlinda mtu mwingine ama mali yanaweza kusababisha kifo.



"Katika mazingira hayo mahakama inaweza kumuona/kupima uwiano wa nguvu iliyotumika ya matumizi ya silaha hatari/tishio," ilibainisha.

# Walimu 18,181 wapata ajira za serikali kwa miaka minne

OFISI ya Rais, Tawala za Mikoa na Serikali za Mitaa (Tamisemi), imesema walimu 18,181 wameajiriwa na serikali kuanzia mwaka wa fedha 2015/16 hadi Machi, mwaka huu.

Hayo yalibainishwa na ofisi hiyo jana bungeni ilipokuwa ikijibu swali la Mbunge wa Mlalo (CCM), Rashid Shangazi. (pichani)

Katika swali lake, mbunge huyo alisema sekta ya elimu nchini inakabiliwa na uhaba wa walimu na kuhoji serikali imeweka mkakati gani wa kuziba pengo hilo la uhaba wa walimu.

Ofisi hiyo ikijibu swali hilo, ilisema idadi hiyo inahusisha walimu wa shule za msingi 10,666, walimu wa shule za sekondari 7,218 na mafundi sanifu maabara 297.

Ilisema serikali itaendelea kuajiri walimu katika sekta ya elimu kwa kadri ya upatikanaji wa rasilimali fedha.

Katika hatua nyingine, Ofisi ya Waziri Mkuu, ilitaja mikakati ya kutatua tatizo la ajira kwa vijana ikiwamo wa Wilaya ya



Kinondoni.

Ilisema mikakati hiyo kuwa ni pamoja na kuwajengea ujuzi kupitia mafunzo ya ufundi stadi kwa lengo la kuwajengea uwezo wa kujiajiri kupitia programu mbalimbali za ukuzaji ujuzi zilizo chini ya Ofisi ya Waziri Mkuu.

Ilibainisha kuwa programu hizo ni uanagenzi (apprenticeship), mafunzo ya uzoefu wa kazi (internship) na kutambua na kurasimisha ujuzi uliopatikana nje ya mfumo rasmi (RPL).

Aidha, uwezeshaji kiuchumi wa vikundi vya vijana kupitia Mfuko wa Maendeleo ya Vijana (YDF) na asilimia 10 ya mapato ya ndani ya serikali za mitaa katika kuwezesha vijana ili waweze kujiajiri ambapo asilimia nne ni vijana, asilimia nne ni wanawake hata vijana wanawake na asilimia mbili kwa vijana wenye ulemavu.

Pia, kuandaa miongozo ya kufundisha masuala ya ujasiriamali kuanzia ngazi ya shule za msingi hadi vyuo vya elimu ya juu.

"Mafunzo haya yanalenga kuwawezesha vijana kuibua miradi na kuitekeleza kwa lengo la kujiajiri na kuweza kuajiri vijana wengine, na kutenga maeneo maalumu ya uzalishaji mali kwa vikundi vya vijana katika ngazi ya halmashauri," ilisema.

Ofisi hiyo ilikuwa ikijibu swali la Mbunge wa Kinondoni (CCM), Maulid Mtulia aliyehoji mikakati ya serikali kuongeza ajira Kinondoni.

# Mradi usambazaji umeme wabuniwa

SERIKALI imebuni mradi wa 'Peri Urban' utakaosambaza umeme katika maeneo yaliyopo pembezoni mwa miji na vijiji nchini.

Wizara ya Nishati ilitoa majibu hayo bungeni jana ilipokuwa ikijibu swali la Mbunge wa Viti Maalum(CCM), Bernadeta Mushashu.

Katika swali lake, Mbunge huyo alisema Manispaa ya Bukoba ina kata na vijiji vingi na wakazi wake ni wakulima na wavuvi, lakini maeneo hayo hayakupatiwa umeme kupitia mradi wa Umeme Vijijini (REA).

"Je, ni lini vijiji hivyo vya green belt vitapatiwa umeme wa REA?" Alihoji.

Katika majibu ya wizara hiyo, ilisema upembuzi wa awali umekamilika kwa nchi nzima ukiwamo Mkoa wa Kagera na utekelezaji wa mradi unatarajia kuanza Julai, 2020.

"Maeneo aliyotaja mbunge ni kati ya maeneo yatakayopendekezwa kusambaziwa umeme huo," ilisema.

Aidha, ilisema serikali kupitia Shirika la Umeme Tanzania (Tanesco), inaendelea kutekeleza miradi ya kusambaza umeme katika maeneo ya miji, majiji, manispaa, na vijiji ikiwa ni mpango endelevu wa kuunganisha umeme na kuongeza idadi ya wateja.

"Maeneo ya Bukoba Mjini yasiyofikiwa na miundombinu ya umeme yataendelea kusambaziwa umeme katika kipindi cha mwaka 2019/20 na baadhi yake katika kipindi kinachoendelea," ilisema.

Katika hatua nyingine, Mbunge wa Momba (Chadema), David Silinde, amehoji serikali lini itamaliza kusambaza umeme wa REA katika jimbo hilo kwa maeneo ambayo hayajafikiwa na umeme mpaka sasa.

Kwa mujibu wa wizara hiyo, Halmashauri ya Momba ina jumla ya vijiji 72 na kati ya hivyo 37 vimepatiwa umeme kupitia miradi ya Tanesco, REA awamu ya pili na ya tatu inayoendelea.

"Vijiji 35 ambavyo havina umeme vitapata umeme kupitia mzunguko wa pili unaotarajia kuanza mwezi Julai, 2020," ilisema.

Ilieleza kuwa kazi za mradi wa kupeleka umeme kwenye vijiji 35 vilivyosalia katika Halmashauri ya Momba zitajumuisha ujenzi wa njia ya umeme wa msongo wa kilovoti 33 yenye urefu wa kilomita 197.6.

Pia ilisema ujenzi wa njia ya umeme wa msongo wa kilovoti 0.4 yenye urefu wa kilomita 126, pamoja na ufungaji wa transfoma 36 za KVA 50 na 100 na kuwaunganishia huduma ya umeme wateja wa awali 1,427.

"Gharama za mradi ni Sh. bilioni 2.65 na utakamilika mwezi Juni, 2021," ilisema.



Ukurasa 13

## Asasi TCRS ilivyowekeza maarifa kwa Machinga Moro 'wakamea'



Ukurasa 14

## Daraja mwokozi Tambani Mkuranga labomoka tena


# BUFE

IJUMAA MEI 15, 2020

Nipashe

BIASHARA, UCHUMI NA FEDHA


BIASHARA

BOSI WA JPM NYANZA:

# Yuleyule na 'hapa kazi tu' hajabadilika hata chembe

• Alipaisha uzalishaji akiamini'mwizi tumtumbue' • Alikesha siku 3 kiwandani akazijua 'dili' • Mameneja: Wa watu, hapindishi ukweli

**Na Anthony Gervas, MWANZA**



John Masalu ambaye ni Meneja Shughuli wa Ushirika Nyanza, aliyefanya kazi na Rais Dk. John Magufuli. **PICHA: ANTHONY GERVAS**

"HAPA kazi tu!" imekuwa kaulimbiu yake na falsafa yake kikazi. Ni kweli, tangu kumfahamu akiwa katika ulingo wa kisiasa ndani ya Baraza la Mawaziri, wasifu wa uchapa kazi wake umebaki kuwa nembo inayomtambulisha.

Wizara ya Ujenzi, alama ya mafanikio yake kiutendaji, takwimu na matendo yake yalifanyika ndani ya kumbukumbu ya kichwa kwa kiasi kikubwa, aliorodhesha takwimu mbalimbali na marejeo ya maandiko yalichukua nafasi ya ushahidi au uhakiki pekee. Kuna wakati ni hadi katika majibu ya papo kwa hapo bungeni.

Ni simulizi inayoenda mbali katika umahiri, tija na mageuzi makubwa ndani ya wizara nyinginezo alikopitia, ikiwamo yenye dhamana na Ardhi, pia Uvuvi. Ni ushuhuda unaoendelea kuonekana 'hapa kazi tu' katika zama za Serikali ya Awamu ya Tano.

Wasifu mwingine wa kikazi, kitaaluma ni mwalimu na mwansayansi ambaye mfumo wake wa uongozi kimatendo ni mchumi aliyetimia, kwa maana ya kuokoa hasara kwa kile anachokisimamia na wakati huohuo, kuongeza tija katika anachokizalisha.

Chama cha Wachumi cha Marekani (AEA), kinatoa tafsiri ya uchumi kwamba ni elimu ya matumizi ya rasilimali katika mazingira ya uhaba unaiokabiliwa na mahitaji mengi, yanayofanyiwa uamuzi sahihi kukidhi mahitaji kipaumbele kilichopo mbele yao.

> **Hapo ndipo nilipoanza kumfahamu, sababu na mimi niliajiriwa mwaka 1989 Ushirika Nyanza.**

Kimsingi, ikiangaliwa ndio falsafa ya uamuzi mara nyingi anafanya Rais Dk. Magufuli katika utendaji wake wa kila siku, kila rasilimali ikiwamo muda ni kipaumbele kwake.

Hayo ndiyo yanashuhudia katika mengi ya maisha ya kila siku nchini serikalini, hata baadhi ya tija za barabara za ndani ya miji nchi kujengwa.

Lakini kama wanavyosema Waswahili "usione vinalelea, vimeundwa," Nipashe ilifanya 'kiguu na njia' hadi kwenye 'nyayo' zake alikopitia kabla ya utumishi wa kisiasa, kudodosa, je, ni Dk. Magufuli huyu huyu tuliye naye katika wajihi huu wa 'hapa kazi tu?'

Hapo ni katika Ushirika wa Nyanza, jijini hapa Magufuli wakati huo kabla hajawa na sifa ya daktari, alikoajiriwa katika nafasi ya Mkemia Mkuu wa Viwanda, alikotumia taaluma ya kemia, ambayo leo hii ina madarasa iliyoongezewa, akitumia na pacha wake, hisabati na ualimu, kazi yake ya awali.

Mzee Enock Masele, Meneja mstaafu wa Ushirika wa Nyanza, hakuwa mchoyo wa ufafanuzi, akianza kuanika wasifu wake kupitia matokeo ya kazi zake, kwa kueleza ushuhuda wa aliyofanya:

"Wakati hajaajiriwa Magufuli, mafuta viwandani tani moja ya mbegu za pamba ilitoa debe sita tu za mafuta, lakini alipoingia katika nafasi hiyo, alisimamia na kuanza kufanya majaribio ya kuzalisha mafuta hayo ili kuhakiki tani moja ya mbegu inazalisha debe ngapi za mafuta.

"Aligundua tani moja ina uwezo wa kuzalisha mafuta kuanzia debe tisa hadi kumi. Uzalishaji huo wa mafuta ulikuwa ukitegemea ubora wa mbegu na hivyo aliweza kugundua kumbe kulikuwa na wizi wa mafuta uliokuwa ukifanywa na mameneja wa viwanda hivyo wa kanda.

"Aliweza kuwadhibiti (watumishi wadokozi) vikali. Alikuwa akilazimika kukesha kiwandani hadi ahakikishe mbegu zilizozalishwa kulingana na ubora wake zitatoa mafuta kiasi gani," anasimulia Mzee Masele, anayedai kumfahamu vyema Magufuli, msaidizi wake mwandamizi kazini na kijana wake.

Ni mwendelezo wa hoja ambayo, John Masalu, Meneja Shughuli wa Ushirika Nyanza, anaunga mkono kufahamu, naye akiendeleza simulizi ya dokezo la Mzee Masalu, kwa ufafanuzi wake mpya:

"Alianza kufuatilia matokeo ya uzalishaji wa mafuta ya pamba viwandani (ginery) na kuanza kufanya majaribio kilo 1000 ya mbegu ya pamba inaweza kutoa kuzalisha mafuta debe ngapi, mashudu kiasi gani na uchafu wake kiasi gani, mpaka ahakikishe ndipo aondoke kiwandani.

"Magufuli ni mwalimu wa Hesabu na Kemia! Hakupenda uongo wala wizi ndiyo maana hata sasa anaendeleza yale mazuri na msimamo wake wa kuchapa kazi aliyotoka nao Nyanza. Ni mtu asiyejaribiwa, mwenye kumbukumbu

INAENDELEA UK.12

BIASHARA

# Yuleyule na 'hapa kazi tu' hajabadilika hata chembe



Rais Dk. John Magufuli, alipozungumza na wakazi wa Jiji la Mwanza, mahali alikoishi na kufanya kazi. **PICHA: MTANDAO**

**INATOKA UK.11**

asiyesahau hata wale alifanya nao kazi toka huko hadi sasa."

Udadisi wa Nipashe, ulijisogeza mkononi mwa, Sospeter Ndoli, Ofisa Rasilimali Watu wa Ushirika Nyanza, ambaye naye ana yake ya zama hizo alipofikiwa kazini na ugeni wa Mkemia Mkuu Magufuli kwa jukumu maalum.

"Nilianza kumfahamu mwaka 1994 baada ya kuja katika kanda yangu, nikiwa Meneja wa Kiwanda Nyambiti. Tulianza kufanya naye kazi kiwandani ya majaribio ya kuzalisha mafuta, ili ahakiki kwamba tani moja ya mbegu inazalisha mafuta kiasi gani.


"Tulikesha naye siku mbili mfululizo kiwandani, tukamaliza hilo siku ya tatu. Alihakiki kuwa tani moja ya mbegu inazalisha mafuta kuanzia debe nane hadi tisa wakati mwingine debe kumi, kutegemea na kiwango cha ubora wa mbegu yenyewe," anasema na kukakamilisha:

"Hapo ndipo nilipoanza kumfahamu, sababu na mimi niliajiriwa mwaka 1989 Ushirika Nyanza."

**ALIKUWAJE KAZINI?**

Mzee Masele, bosi wa Mafuguli wakati huo, anasema bado imemkaa wasifu anaoukumbuka kwamba: "Alikuwa mwenye msimamo mkali katika kazi, asiyeogopa kusema ukweli hata kwa bosi wake na hakuweza kumung'unya maneno 'alifunguka.' Yeye udanganyifu, uongo ilikuwa ni mwiko kwake, alipenda haki na ukweli ilikuwa ni kazi kazi!"

> **"Magufuli ni mwalimu wa Hesabu na Kemia! Hakupenda uongo wala wizi ndiyo maana hata sasa anaendeleza yale mazuri na msimamo wake wa kuchapa kazi aliyotoka nao Nyanza.**



Mzee Enock Masele, alikuwa Meneja Mkuu, anayemwongoza Rais Dk. John Magufuli. **PICHA: ANTHONY GERVAS**

Anasema, aina ya uchapakazi aliyokuwa nao katika Ushirika Nyanza, haujabadilika hadi sasa na alifanya kazi kwa ushirikiano na wafanyakazi wenzake, bila ya kubagua hali ya unyonge wa mtu.

Mzee Masele anakumbusha sifa yake kwamba, alikuwa anatoa mapendekezo kwenye uongozi wenye tija na mara nyingi walioangukia katika ubadhirifu au wizi wa mali za Ushirika Nyanza, hakuwa na masihara nao alitaka wafukuzwe kazini.

Ni aina ya msimamo wa kiongozi anaoendeleza sasa kwa watendaji kazini serikalini, ambao ama 'wanatibuliwa' kazini au ikiendana na hatua zingine za kisheria, kunapokuwapo ushahidi wa hujuma na ubadhirifu.

Meneja huyo mstaafu wa Nyanza, anamsifu Magufuli kuchangia kuongeza mapato ya Ushirika Nyanza, kupitia mafuta ya pamba yaliyouzwa ndani ya ushindani mkubwa sokoni, ikishinda mafuta mengine katika Soko la Kanda ya Ziwa, mikoa na nchi jirani kama Uganda na Rwanda.

Katika sifa hizo za kazini, Masalu anaongezea kwamba Magufuli aliipenda sana kazi yake, akiwa na hulka ya uadilifu na hakupenda kudanganywa na kutokuwa na makuu kazini, daima hakuwa mchelewaji kazini, wakati huo alikuwa mkazi wa jijini Mwanza.

Huku akimsifu kwa utanashati, aliyopenda kuvaa suti na saa, anasema mapambano dhidi ya ubadhirifu wa mafuta ya Ushirika Nyanza, yalizaa matunda tabia ya kiutendaji, wafanyakazi wa chini walimuiga uadilifu, ukweli na uaminifu kazini.

**MAISHA KIJAMII?**

Masalu kijamii anamtaja alikuwa 'mtu wa kujichanganya' na watu bila kubagua, ingawaje daima hakuonyesha dalili zozote za mambo ya siasa, aliyoyaibukia baadaye.

Kwa mujibu wa Masalu, Dk. Magufuli alionyesha upenzi wa mpira wa soka wakati huo, japo hakuweza kufahamu timu aliyoishabikia, wakati huu Mwanza ilikuwa na vilabu vya Pamba na Toto, Co-op, mbali na 'vigogo' Simba na Yanga za Dar es Salaam.

Kwa sasa vilabu hivyo vya soka vya Mwanza, vilivyowahi kutikisa kandakanda kila nchi, vimefifia.

Ilikuwaje mwanasayansi huyo, mwalimu na 'jembe' la uzalishaji kwa Ushirika Nyanza, alijitosa kwenye siasa na leo hii ndio amekabidhiwa dhamana ya kuiongoza nchi, katika awamu ya kwanza ya urais tayari akiwa na makuu, baada ya wastani miaka 20 ya uwaziri wenye mafanikio 'A -Z'?

Nipashe, ilirejesha swali kwa Mzee Masele, Meneja Mkuu wa Ushirika Nyanza, ambaye michakato baada ya kazi ya ualimu imepitia mkononi mwake.

Anaanza na historia alivyoajiriwa Dk. Magufuli katika Ushirika Nyanza mwaka 1989, akiwa Mkemia Mkuu wa Viwanda vya 'Ginery' (vya kuchakata mafuta ya pamba) na mwaka mmoja baadaye, 1990 aliomba ruhusa kwenda kugombea ubunge jimboni Biharamulo Mashariki, lakini kura hazikutosha, akarejea kazini.

Mzee Masele anasimulia mwaka 1995, Dk. Magufuli aliomba ruhusa tena kugombea ubunge katika Jimbo la Chato mkoani Geita, alikosema ameitwa na wananchi kwenda kugombea nafasi hiyo, kisaidia maendeleo an akafanikiwa, baadaye anateuliwa kuwa Naibu Waziri wa Ujenzi. Ukawa ndio mwisho wa safari yake Nyanza.

***Mwandishi wa makala hii anapatikana kwa anwani ya barua pepe: anthonygervas@yahoo.com na simu: (+255) 0682 869 244, Kanda ya Ziwa.***

BIASHARA

MRADI WA MILIONI19/-

# Asasi TCRS ilivyowekeza maarifa kwa Machinga Moro 'wakamea'

• Manispaa yatia mkono wa mafanikio; walengwa kilio chao leo ni corona

**Na Christina Haule,** Morogoro

SHIRIKA la Kikristu la Kuhudumia Wakimbizi la Tanganyika (TCRS), ofisi ya Morogoro, limeamua kujisogeza kuchangia shughuli za ujasiriamali mkoani ikiwa na thamani ya shilingi milioni 19 kwa wafanyabiashara ndogo maarufu kama wamachinga.

Waliangukiwa na neema hiyo kuanzia mwaka 2017 hadi sasa, kama inavyoelezwa na Gasper Werema, Ofisa Mwezeshaji wa TCRS, akitaja jumla yao ni 226 kutoka vikundi vya kata 10 za Manispaa ya Morogoro.

Werema, ambaye ni Meneja Msaidizi, anasema lengo la mradi huo wa miaka minne ni kuwasaidia machinga 250 na imeshawasajili wanawake 80 na wanaume 146 waliopata mafunzo kwa awamu tatu mfululizo kuhusu ujasiriamali na maendeleo endelevu.

Werema anataja makundi ya kitaalamu ya wanufaika ni biashara wa ushonaji, utengenezaji sabuni za maji, mifuko ya karatasi na huduma za saluni za kike na kiume.

**WALENGWA**

Katibu wa kikundi cha watu 23 kilichopo Kihonda jijini Morogoro, Aloyce Mwakukui, anasema walianza kutengeneza bidhaa za ngozi, viatu na mikoba ya kinamama wakiwa na mtaji mdogo na uliowakwamisha kufikia malengo waliyokusudia.

Anasema, TCRS liliwaunga mkono mtaji na ujuzi wakatengenezaji viatu kama vile ngozi, misumari, gundi na vingine vingi vyenye thamani ya shilingi 850,000 bado wanakubaliana na ugumu wa biashara, kutokana na ushindani mkubwa wa bidhaa za ngozi sokoni, sambamba na mzunguko wa fedha kusuasua.

"Nionavyo wananchi walio wengi kwa sasa wameelemea kwenye kununua bidhaa za vyakula, viatu na mikoba imekuwa kama anasa kutokana na ugumu wa upatikanaji wa fedha ulivyo kwa sasa miongoni mwa wananchi walio wengi," anasema Mwakukui.

Anaeleza matarajio yao, kwamba baada ya kupungua janga lililopo la corona dhidi ya nyendo za uchumi na biashara, matarajio ni kukuza mtaji wao wazalisha bidhaa za kandambili kila siku, baada ya kuajiri wafanyakazi watakapofikia hadhi ya kampuni ndogo.

Kassim Ally, mjasiriamali na Katibu wa Kikundi cha Wajasiriamali cha Msimamo kilichopo Kata ya Mwembesongo, mjini hapa kinachojishughulisha na utengenezaji sabuni za maji, anasema kwao biashara sio mbaya katika msimu huu kwa kuwa kuna uhitaji mkubwa wa bidhaa hiyo kwa sasa.



Meneja Msaidizi wa TCRS, Gasper Werema (kulia), akiwaelekeza jambo wanakikundi cha ujasiriamali cha kutengeneza sabuni za maji kinachoitwa Msimamo Group, kilichopo Kata ya Mwembesongo, mjini Morogoro. **PICHA: CHRISTINA HAULE**

Ally anasema, soko lao ni kupitia mitaani wanakotembeza, anakokiri wanakumbana na ushindani, ikizingatiwa sabuni yao ni ya kiwango cha chini na wanaelemewa bei.

"Sisi tunatengeneza sabuni nzuri na kuuza kwa lita moja shilingi 1,200 hadi 1,300, lakini wapo wengine wanatengeneza bila ubora na kuuza shilingi 1,000 na kusababisha kuharibu soko la biashara hiyo," anaeleza Ally.

Washona nguo wa kikundi cha Muungano wa Vijana Wajasiriamali Chamwino (MUVIWACHA) wanaishukuru TCRS, kwa msaada wa vyerahani viwili na malighafi za kutengenezea batiki, iliyowawezesha kupiga hatua ndani ya changamoto ya kiabiashara, hasa kipindi kilichopo cha janga la corona.

Katibu wa kikundi hicho, Azizi Abeid, anasema wameendeleza biashara kwa kutengeneza batiki na kushona magauni waliyoyauza ndani ya manispaa na wilaya za mkoa wa Morogoro, kulingana na mwingiliano wa masoko yao ya minada.

Anasema, pia wanalima na TCRS imewasaidia vifaa vya kilimo iliyowasaidia katika uzalishaji wa mboga na matunda.

Hassan Abeid, ni mjumbe wa kikundi hicho, anayesema changamoto walio nayo sasa ni biashara kuingiliwa na corona anaiomba TCRS kuwasaidia elimu na malighafi ili waweze kutengeneza vitakasa mikono na viuadudu (sanitizer).

Anasema itawawezesha kuendana na mahitaji ya soko kwa wakati uliopo, kwani biashara zingine zimerudi nyuma, hata wakashindwa kuendelea kutengeneza nguo, soko likiwa limekufa.

**MWENYEKITI MACHINGA**

Mwenyekiti wa Shirika la Umoja wa Wafanyabiashara ndogo 'Machinga' (SHIUMA) Mkoa wa Morogoro, Faustine Francis, anasema licha ya mafanikio ya wafanyabiashara katika Manispaa ya Morogoro, bado kuna ugumu wa kibiashara.

Anataja ni wa kupata mikopo ambayo sehemu kubwa ya Machinga wana mitaji midogo, hivyo hutegemea kwa ajili ya kuendesha maisha ya kila siku.

Francis anaishukuru serikali mkoa wa Morogoro, kwa kushirikiana na mashirika kama TCRS, zimejitahidi kuondoa changamoto za wafanyabiashara wadogo katika vikwazo kama mikopo wanayoihitaji.

Anasema elimu waliopewa wajasiriamali kuheshimu kanuni za biashara na sheria za manispaa, zimewasaidia kuendesha biashara, tofauti na mwanzo, ila ugumu uliopo sasa ni maradhi ya corona yaliyowaharibia wateja soko na katika magulio.

"Baadhi ya wakulima wa mazao ya chakula, mboga mboga na matunda wanaogopa kuingia mjini kwa sababu ya hofu ya corona. Hali hiyo inawafanya wafanyabiashara wangu wa bidhaa hizo kuzipata kwa shida na kuuza kwa shida kutokana na kupungua kwa wateja kutokana na watu walio wengi kutoingia mjini," anasema Francis.

Anasema hata baadhi ya bidhaa za dukani kama vile za mitumba zilizonunuliwa na Machinga na wakazichuuza mitaani, pia zimeadimika kiasi.

> "Soko lao ni kupitia mitaani wanakotembeza, anakokiri wanakumbana na ushindani, ikizingatiwa sabuni yao ni ya kiwango cha chini na wanaelemewa bei.

**OFISA BIASHARA**

Festus Herman, ni Ofisa Biashara wa Manisapaa ya Morogoro, anasema wanaendeleza kuwasaidia wafanyabiashara wadogo kwa mikopo kupitia bajeti za halmashauri kupitia mikopo ya kisheria; asilimia nne ya bajeti yao kwa vijana na wanawake

Herman anatoa rai kwa wafanyabiashara wawe wepesi kwenda katika maeneo yanayoelekezwa, ili waondokane na dhana ya kutaka kukaa katikati ya miji, kwa kuwa miji inapanuka, pia wajiunge katika vikundi wanufaike na fursa za mikopo.

Msimamizi wa Miradi ya TCRS mkoani Morogoro, Rehema Samwel, anasema wamejizatiti kushirikiana kwa karibu na serikali kutatua changamoto zinazotarajiwa ili wawatoe katika ngazi waliopo sasa.

Rehema anasema, tathmini ya wafanyabiashara wadogo katika mikoa ya Morogoro, Dar es Salaam na Dodoma iliyofanywa na TCRS kwa kushirikiana na Chuo Kikuu Huria cha Tanzania (OUT) umehudumia vijiji zaidi ya 25 ndani ya kata sita za Wilaya Morogoro tangu mwaka 2005.

Anazitaja vijiji hivyo kuwa ni Mkuyuni, Mvuha, Selembara, Mtamba, Lundi na Mkulazi na kwa kuwasaidia kwa huduma mbalimbali, zikiwamo misaada ya chakula wanapokutwa na njaa. Januari mwaka 2019, shirika hilo lilianza kutoa huduma katika kata mpya za Kiroka, Tomondo na Mikese na kufanya misaada yake kufikia vijiji 35.

TCRS lenye makao yake makuu jijini Dar es Salaam, lilianzishwa mwaka 1964 ikiwa ni programu ya nchi kutoka shirikisho la Kilutheri duniani na kwa wakimbizi wenye dharura.

UCHUMI

# Daraja mwokozi Tambani Mkuranga labomoka tena

**Na Yasmine Protace,** MKURANGA

- Historia ya mateso miaka 20 yarejea
- Kuogolea au kutumia madumu 500/-

WAKAZI wa mahali hapo wana kumbukumbu ya adha ya kero iliyowakabili, kukosa daraja. Mahali hapo panafanana na hadhi ya mpakani; Namanga, Mutukula ya Tunduma, nako kunaitwa Mto Tambani kunakotenganisha mkoa wa Dar es Salaam na Pwani, wilayani Mkuranga. Tofauti yake, uhitaji kuwa na pasipoti kutoka upande mmoja hadi mwingine.

Hapo mahsusi kunakotajwa ni kwenye daraja la Kifaulo lililopo Tambani Mkuranga. Wakati maduka mengi yako ng'ambo ya Dar es Salaam, mvua ziliponyesha, palikuwapo mafuriko na mtihani wa kuvuka kati ya upande mmoja na mwingine.

Waliolazimika kuvuka, ama walikubali kuogelea, kuvushwa kwa 'mitumbwi pori' ya madumu yenye adha na madhara lukuki au walishindwa kabisa kuvuka.

Ni matokeo ya kuharibika mto huo mwaka 1998, kutokana na mvua kubwa za Elinino, hata wakahamia katika adha ya kusaidiwa.

Waliovushwa iliwagharimu Sh. 500. Hicho kikageuka kilio cha wanakijiji wakiomba msaada wapatiwe ufumbuzi wa daraja la kuwawezesha kuvuka waione Dar es Salaam, ambako mbali na maduka na mahitaji ya tiba, kuna shule wanakosoma watoto.

Adha hiyo iliyodumu kwa miaka 20, ilifika hatua mvua ziliponyesha, wazazi waliwazuia watoto wao kwenda shule kutokana na kuhofia usalama wao.

Hapo ndipo wakalifanya ombi maalum kwa mbunge wao na uongozi wa wilaya na walifanikiwa mwaka juzi kupata ufadhili wa zaidi ya Sh. milioni 500 kwa ajili ya kujenga daraja, ambayo mafanikio yake kukawapo daladala kati ya Kariakoo na Tambani, kwa nauli ya Sh. 600. Sasa kulikoni? Baada ya wanakijiji kupumua wastani wa siku 1,000 sasa, janga la mvua limeridhisha uhalisiwa wa historia palepale.



Boti linalowavusha wakazi wa Tambani Mkuranga. **PICHA ZOTE: YASMINE PROTACE.**

#### DARAJA LABOMOKA

Ni taarifa mbaya, ukombozi wa adha ya miaka 20 kubomoka daraja la Tambani, imerudia historia yake, mvua kubwa za mwaka huu zimesababisha kuharibika tena daraja na wananchi kurudia kilichojiri katika historia, ikiwamo kuvushwa kwa madumu, mto ukifurika.

Ofisa Mtendaji wa Kijiji cha Tambani, Gasper Patrick, anasema awali kabla ya kutengenezwa daraja, wanakijiji walikuwa wachache, lakini baada ya kutengenezwa watu wengi walihamia kijijini hapo na kukajengwa vibanda vingi vya biashara.

"Watu walihamia wengi, wamejenga maduka makubwa ya biashara, lakini tokea mvua iharibu miundombinu, baadhi ya wafanyabiashara wamefunga maduka yao," anasema Patrick.

> **Watu walihamia wengi, wamejenga maduka makubwa ya biashara, lakini tokea mvua iharibu miundombinu, baadhi ya wafanyabiashara wamefunga maduka yao.**



Wakazi wa Tambani Mkuranga, wakivuka mto Kifaulongo, kuelekea jijini Dar es Salaam, kwa mfumo wa kivuko uliopo sasa

Anafafanua kuwa waliohama kijijini wengi wamerejea jijini Dar es Salaam walikotoka, sababu kuu ni kuharibika mawasiliano ya daraja, kwani gharama ya mbadala wa usafiri bodaboda kwa asiyeweza kuogelea ni kubwa sana.

Kwa mujibu wa Patrick, msafiri huyo analazimika kupitia Mbande kwa kulipa kati ya Sh. 2500 na Sh. 3,000 huku wanaotumia madumu kuvuka, wanalipa Sh. 300, anasema kulikuwapo na boti lililowavusha, lakini sasa limeharibika.

Mwajuma Ally, ni mwanakijiji wa Tambani, anasema ni adha inayowakwaza wanapotaka kwenda hospitali na hasa usiku, inakuwa changamoto kwao ya usafiri.

Mwenyekiti wa Kijiji, Amir Mbamba, analalamika kwamba kulipokuwapo na daraja, kijiji kilifanikiwa kupata wakazi wapya wengi waliofika kuwekeza na daraja ilipobomoka, anakiri wengi wamehama ghafla.

Amiri anasema, kivunjika daraja hilo ni hali inayoendana na wakazi wa Tambani kuyumba kiuchumi na kibiashara, kwani mawasiliano ya usafiri yamekuwa na msaada mkubwa kwao.

Mwenyekiti huyo anatoa mfano wa wafanyabiashara kupandisha bei za bidhaa zao, akifafanua: "Kuharibika kwa daraja, wafanyabiashara ambao wanaagiza bidhaa kutoka jijini Dar es Salaam, wamekuwa wakipandisha bei bidhaa zao kwa madai kwamba wanaingia gharama kubwa kuingiza bidhaa."

#### MBUNGE AGUNA

Omary Kisato, Katibu wa Mbunge wa Mkuranga, anasema Mbunge Ulega hadi sasa ameomba msaada wa boti mbili wazipeleka katika vijiji viwili jirani; Tambani na Nasibugani.

"Kutokana na mvua kunyesha na kuharibu maeneo hayo, mbunge aliomba boti na alifanikiwa kupata boti mbili," anathibitisha katibu huyo.

Pia, kuhusu kuharibika daraja lingine la Kifaulongo, Mbunge Ulega, alituma timu ya watu kwenda kukagua uharibifu na namna lilivyoharibika na katika mashauriano, ni kwamba baada ya mvua kwisha madaraja yaliyoharibika yatajengwa kwa chuma.

#### DED MKURANGA

Mkurugenzi Mtendaji wa Halmashauri ya Wilaya Mkuranga, Injinia Msham Munde, anakiri mvua zinazoendelea kunyesha zimeharibu miundombinu mingi ya mawasiliano katika vijiji vyake, hata kuchangia kuharibika kwa miundombinu muhimu ya usafiri.

Katika daraja la Kifaulongo ambako ni kiungo cha Mkuranga na Mbande, Injiani Munde ana ufafanuzi: "Tarura (Mamlaka ya Usafiri wa Vijijini) imefika katika tukio na kuomba fedha. Mvua zitakapoacha kunyesha daraja la Kifaulongo litatengenezwa pale palipoharibika."

Katika mkutano wa Mbunge wa Mkuranga, Abdallah Ulega uliofanyika mwaka juzi na wakati wa Tambani Mkuranga, wanakijiji waliomba wawekewe daraja ili waache kuogelea pale kipindi mvua zinaponyesha.

Wanakijiji hao katika mchango wao, alisema tangu kunyesha mvua za elnino za mwaka 1998 ziliponyesha na kusababisha daraja kukatika, walipata shida kuvuka mto mvua ziliponyesha na walilazimika kuvushwa kwa mitumbwi ya asili, wakilipa Sh. 500 na wanafunzi wakitozwa Sh. 200.

Wakazi hao walidai wakati huo waliozunguka walilazimika kulipa bodaboda kati ya Sh.7,000 na Sh. 5,000, kutoka Mbande, Dar es Salaam hadi Tambani, Mkuranga.

Hapo ndipo Mbunge Ulega aliwaeleza wapigakura wake kwamba serikali ilishasikia kilio chao na kuwatengea bajeti ya Sh. milioni 500 kwa wakati huo, ambayo ndio iliwezesha kujengwa daraja hilo lililobomoka.



## Serikali yaandaa miongozo corona wenye ulemavu

**Na Paul Mabeja, DODOMA**

SERIKALI imeandaa miongozo mbalimbali kwa ajili ya watu wenye ulemavu kusaidiwa kupambana na maambukizo ya ugonjwa wa corona.

Hayo yalibainishwa jana na Naibu Waziri, Ofisi ya Waziri Mkuu anayeshughulikia watu wenye ulemavu, Stella Ikupa, alipokuwa akikabidhi msaada wa vifaa vya kukabiliana na ugonjwa huo kwa Shirikisho la vyama vya watu wenye ulemavu Tanzania (Shivyawata).

Alisema miongozo hiyo imezingatia wakati huu mataifa mengi dunia yanaangalia namna bora ya kukabiliana na ugojwa huo.

"Kwa mfano kuhakikisha wanapata vifaa vya kunawia ambavyo vimeboreshwa na kuwa jumuishi kwa watu wenye ulemavu, hivi leo nimekabidhi ndoo za kunawia mikono na mashine maalum ya kunawia pasipo kutumia koki 'Free Hand Water Tape'," alisema.

Naibu Waziri huyo alisema serikali inatambua mchango wa watu wenye ulemavu na ndio maana viongozi na wadau mbalimbali wamekuwa wakijitokeza kusaidia kwenye mapambano dhidi ya janga la corona bila kusahau namna ya kuwasaidia na kuweka mazingira wezeshi ya kukabiliana na ugonjwa huo.

"Nikiwa kama mdau nimeona umuhimu wa kukabidhi ndoo za kunawia mikono 90 na mashine maalum ya kunawia bila kutumia koki kwa ajili ya kusaidia watu wenye ulemavu katika mikoa 10 ikiwamo Dar es Salaam, Dodoma, Kilimanjaro, Arusha, Mwanza, Tanga, Pwani, Iringa na Morogoro," alisema Ikupa.

Alitoa wito kwa kundi hilo maalum kuendelea kufuata maelekezo yanayotolewa na viongozi na wahudumu wa afya pamoja na kujenga tabia ya kusoma taarifa kwenye mitandao ya kijamii na meseji wanazopata kupitia simu zao za mkononi kukabiliana na Covid-19.

Aliwataka wadau mbalimbali wenye nia njema kuendelea kujitokeza na kuunga mkono juhudi za serikali kukabiliana na janga la ugonjwa wa corona nchini.

Naye, Katibu wa Shivyawata Mkoa wa Dodoma, Justus Ng`wantalima, alimshukuru kiongozi huyo kwa kutambua watu wenye ulemavu na kuamua kutoa msaada wa vifaa hivyo ambavyo ni rafiki kwa watu hao.

Alieleza kuwa vitawafikia wenye ulemavu wengi nchini na watanufaika kwa kujikinga na virusi vya corona.

"Haimaanishi kama mtu ana ulemavu basi hawezi kupata maambukizo ya ugonjwa huu wa corona, ugonjwa huo unaweza kumpata mtu yeyote hivyo uwapo wa vifaa hivi utasaidia watu wenye ulemavu kujikinga na janga hilo," alieleza Ng'wantalima.

# DC awataka wananchi kuzingatia uvaaji barakoa

**Na Paul Mabeja, KONGWA**

MKUU wa Wilaya ya Kongwa mkoani Dodoma, Deogratius Ndejembi, amewataka wananchi kuendelea kuzingatia uvaaji wa barakoa, kila wanapokwenda ili kujikinga na maambukizo ya virusi vya corona.

Ndejembi, aliyasema hayo jana ofisini kwake, wakati alipokuwa akipokea msaada wa vifaa mbalimbali vya kujikinga na maambuzo ya virusi vya corona (Covid-19) kutoka shirika lisilokuwa la kiserikali la GFF.

Alisema matumizi ya barakoa sasa kutokana na maambukizo ya ugonjwa huo kusambaa nchini wananchi hawana budi kuendelea kuzingatia uvaaji wake ili wajikinge na corona.

"Kuwafungia watu ndani siyo suluhisho kinachotakiwa kuzingatiwa na wadau mbalimbali ni utoaji wa elimu, ili wanachi waendelee kuzingatia maelekezo na kutumia vifaa vitakavyo wakinga wasiambukizwe ugonjwa wa corona," alisema Ndejembi.

Vile vile, Ndejembi alisema wananchi hawatakiwi kuchagua maeneo ya kuvaa barakoa bali wavae kila eneo wanalokwenda ili kusaidia kupunguza uwezekano wa kuongezeka kwa maambukizo mapya nchini.

"Lazima viongozi muwaeleze wananchi wetu kuwa barakoa siyo jambo la hiari bali ni lazima kila anapokwenda mwananchi avae iwe mnadani au gulioni kwa kuwa vitambaa vya kushona barakoa vipo hata vitenge vya nyumbani vitumike kushona," alifafanua Ndejembi.

Alishukuru shirika hilo kuwapatia msaada huo ambao utasaidia kuongeza nguvu ya mapambano dhidi ya virusi vya corona.

"Tunashukuru sana GFF, kwa msaada huu wa hivi vifaa vitatusaidia sana katika mapambo dhidi ya corona na nitowe wito kwa wadau wengine kujitokeza kufanya kama ambavyo mmefanya nyie hii leo hapa Kongwa," alisema.

Naye, Mkurugenzi Mtendaji wa Shirika la GFF, Aisha Msantu, alisema wametoa msaada huo ikiwa ni katika kuunga mkono jitihada zinazofanywa na serikali kwenye mapambano dhidi ya ugonjwa wa corona.

Alisema vifaa walivyotoa ni ndoo za kunawia mikono kwa maji tiririka, sabuni pamoja na vitakasa mikono ambavyo wilaya itavigawa katika taasisi mbalimbali pamoja na maeneo mengine yenye mikusanyiko.

"Msaada huu tumeuleta leo hapa ili kuunga mkono juhudi za serikali katika mapambano dhidi ya ugonjwa huu wa corona nchini ambao umeleta athari kubwa ya kiuchumi kwa taifa na dunia kwa ujumla," alisema Msantu.

Vile vile, alisema Wilaya ya Kongwa imekuwa ya kwanza kupata msaada huo ambao pia utaendelea kutolewa katika maeneo mengine ya mkoa wa Dodoma, ili kusaidia wananchi kukabiliana na virusi hivyo.

Kwa upande wake, Mkurugenzi wa Halmashauri ya Wilaya ya Kongwa, Omary Mkulo, alisema watahakikisha vifaa hivyo vyote vinafika katika maeneo husika ili kusaidia mapambano dhidi ya virusi hivyo.

"Tunashukuru sana kwa kupata dhana hizi ili kutuwezesha kuingia vitani kwa kuwa hata taifa lilipoingia katika vita na Nduli Iddi Amini kuna watu kama nyie walitoa msaada wao ili kuwezesha vita vile, hivyo vifaa hivi vitakua silaha tosha kupambana na corona hapa Kongwa," alisema Mkulo.




Mkazi wa Jiji la Dodoma, akilikokota tolori alilolisheheni matenga matupu na kumfanya ashindwe kuona nyuma katika Barabara ya Soko Kuu la Majengo, jana, kitendo ambacho ni hatari kwa usalama barabarani. **PICHA: PETER MKWAVILA**

# Wadau waombwa kusaidia wasiojiweza

**Na Peter Mkwavila, DODOMA**

WADAU mbalimbali wameaswa kuwasaidia chakula watu wasiojiweza katika mfungo wa Mwezi Mtukufu wa Ramadhani ili kuwapunguzia makali ya kukosa chakula.

Wito huo ulitolewa jana jijini hapa na Shekhe wa Ahmadiyy Musilimu Jamaat Tanzania, kutoka jijini Dar es Salaam, Bashart ut Rehman Butt, alipokuwa akizungumza na waandishi wa habari.

Alisema ni vyema wakati huo wa mfungo, taasisi, mashirika mbalimbali, watu binafsi na madhehebu ya dini kusaidia watu hao.

"Kipindi hiki cha mfungo wa Mwezi Mtukufu wa Ramadhani, kuna makundi ya watu wasiojiweza ambao wamefunga na hawana uwezo, wanatakiwa kusaidiwa misaada mbalimbali ili kuwapunguzia makali," alisema.

Alisema taasisi, mashirika na watu binafsi wana wajibu mkubwa ya kuwaangalia makundi hayo maalumu kwa jicho la huruma ili na wao kujikimu kupitia misaada hiyo itakayotolewa.

Aliwataka waumini ndani ya misikiti pia kujitoa kwa mali zao, na kufanya Ibada kwa unyenyekevu huku wakiwatendea haki wengine ambao wana hali ngumu ya maisha.

Alisisitiza waumini kuzingatia mafundisho wanayopewa kwenye mwezi huo na kuhakikisha wanaendelea kuyatenda hata baada ya kumalizika kwa mfungo huo.

Katika hatua nyingine, Shekhe huyo aliwahimiza Watanzania kuendelea kuomba kwa Mungu kuwaepusha na maambukizi ya virusi vya corona.

"Corona ipo na tunatakiwa tuchukue tahadhari kubwa tena kwa vitendo ikiwa kuvaa barokoa na kunawa na maji tiririka na sabuni pamoja na kupaka vitakasa mikono," alisema.





## Wanawake waonywa kutumiwa na wanasiasa

**Na Grace Mwakalinga, MBEYA**

WANAWAKE mkoani Mbeya, wametakiwa kuepuka kutumiwa na wanasiasa kipindi hiki cha kuelekea uchaguzi mkuu, kama daraja la kuwavusha.

Badala yake wanawake hao wameshauriwa kuwashawishi wanasiasa kuwainua kiuchumi.

Angalizo hilo lilitolewa jana na Diwani wa Mshewe, Esther Mbega, wakati akizungumza na Nipashe juu ya jitihada alizozifanya katika kuwahamasisha wanawake kujitokeza na kugombea nafasi mbalimbali za uongozi.

Alisema imekuwa ni kawaida wanasiasa kuwatumia wanawake kujinufaisha hasa kupata madaraka na kusahau kuwa bila kundi hilo wasingepata badala yake wanaanza kuwadharau.

Alisema endapo kundi hilo muhimu kwa taifa litaendelea kukubali kutumiwa na wanasiasa, litaendelea kuwa masikini na kulalamikia hali ngumu ya maisha huku wanasiasa wakizidi kuchanua.

Mbega aliwashauri wanasiasa wanaowatumia wanawake wenzake kipindi cha kampeni za kisiasa na kuwaacha baada ya kupata wanachokitaka kuacha tabia hiyo.

Aliwataka wanasiasa hao na badala yake wajikite katika kuwahamasisha kuunda vikundi vya ujasiriamali na kuwapatia mitaji.

"Mkiendelea kutumika na wanasiasa, mtaendelea kuwa maskini wakati wenzenu wanazidi kuwa matajiri kwa kupitia migongo yenu, hivyo nashauri tuendelee kufanya shughuli zenu kwa maslahi ya familia zetu, wakitaka waje watusaidie mitaji," alisema Mbega.

Aidha, aliwataka wanawake kutumia fursa mbalimbali za kiuchumi kwa kuhakikisha wanawekeza kwenye uzalishaji wa bidhaa mbalimbali zenye ubora ili kuunga mkono juhudi za serikali za kufikia uchumi wa viwanda.

Aliwataka wanawake kuwa mstari wa mbele kuwekeza hata kama wana umri mkubwa kwa madai kuwa kundi hilo ndilo lenye jukumu kubwa la kulea watoto.

Aliongeza kuwa wanawake wanatakiwa kuwa na nidhamu ya matumizi ya fedha wanazopata ili kuendeleza biashara zao badala ya kuwa na matumizi makubwa kuliko kile wanachozalisha kitu ambacho alidai kinasababisha watu wengi kufilisika.

Mkurugenzi wa Jiji la Mbeya, James Kasusura, alisema miongoni mwa vikwazo vinavyorudisha nyuma jitihada za wanawake ikiwamo shughuli za biashara ni kukosa mtaji.

Alisema licha ya vikwazo baadhi ya wanawake bado muitikio wao ni mdogo kujiunga kwenye vikundi ili kupata fursa ya kukopesheka na taasisi za kifedha pamoja halmashauri.

# Kada wa Chadema kortini kesi ya uhujumu uchumi

**Na Grace Mwakalinga, MBEYA**

KADA wa Chama cha Demokrasia na Maendeleo Chadema, Mdude Nyagali, amefikishwa katika Mahakama ya Hakimu Mkazi, Mkoa wa Mbeya ambako amesomewa shtaka moja la uhujumu uchumi.

Mshtakiwa ambaye ni mkazi wa Kata ya Itezi jijini Mbeya juzi alipandishwa kizimbani ili kusomewa shtaka hilo baada ya kukutwa na gramu hizo za dawa za kulevya aina ya heroine nyumbani kwake.

Akimsomea shtaka lake mbele ya Hakimu Mkazi Mkoa wa Mbeya, Zawadi Laiser, mwendesha mashtaka wa serikali, Wakili Mwandamizi Basilius Namkambe akisaidiwa na Wakili wa Serikali, Lugano Mwakilasa, alidai kuwa mshtakiwa alikamatwa Mei 10, mwaka huu akiwa nyumbani kwao maeneo ya Itezi.

Wakili wa Serikali, Namkambe aliiambia mahakama kuwa kitendo hicho ni kinyume cha kifungu namba 15 (A) kifungu kidogo cha kwanza cha sheria namba tano ya kudhibiti dawa za kulevya ya mwaka 2015 kama ilivyofanyiwa mabadiliko yake ikisomwa pamoja na kifungu cha 23 cha jedwali namba moja.

Baada ya kusomewa mashtaka yake, mshtakiwa hakutakiwa kujibu chochote kwa kuwa mahakama hiyo haina mamlaka ya kisheria ya kusikiliza shauri hilo na mtuhumiwa amepelekwa rumande mpaka Mei 27, mwaka huu kesi hiyo itakaposomwa tena.



Baadhi ya wakazi wa Mtaa wa Manga-Veta, Kata ya Ilemi katika Halmashauri ya Jiji la Mbeya, wakitupa taka kwenye dampo la halmashauri hiyo, lenye mrundikano wa takataka na kutelekezwa bila ya kuondolewa kwa miezi miwili sasa, licha ya watendaji wa mitaa na wenyeviti kutoza kila familia Sh. 1,000 kwa mwezi kama gharama ya shughuli hiyo. **PICHA: GRACE MWAKALINGA**

# Mtafiti atoa somo umuhimu wa ulaji wa vyakula vya asili

**Na Innocent Ng'oko, MBEYA**

MTAFITI na mzalishaji wa vyakula vya asili, Prof. Dorcas Kibona, ameziomba Wizara za Afya na Kilimo kuandaa mpango wa kuwahamasisha Watanzania kula vyakula vya asili ili kulinusuru Taifa.

Alisema kwamba kwa kufanya hivyo, itasaidia huondokana na wimbi la watu wenye matatizo yatokanayo na kula vyakula visivyo na ubora.

Kauli hiyo ilitolewa jana na Prof. Kibona wakati akizungumza na gazeti la Nipashe juu ya umhimu wa kula vyakula vya asili ambavyo vinamsaidia mtu kuwa na afya bora.

Alisema vijana wengi kwa sasa hawana utamaduni wa kula vyakula vya asili, jambo ambalo linatilia shaka katika uwezo wao wa kiakili na kiafya katika kufanya maamuzi sahihi ya maendeleo ya nchi.

"Kuna wimbi la vijana wengi hususani wa maeneo ya mijini kutokuwa na utamaduni wa kula vyakula vya asili, hiyo inatia hofu kuona kundi la vijana ambao ndiyo nguvu kazi ya nchi hawatilii maanani vyakula vya asili licha ya kuwa na umhimu katika afya zao," alisema msomi huyo.

Alisema taifa lolote likiwa na watu goigoi kutokana na kutotilia mkazo wa vyakula vya asili ni hatari kwa maendeleo ya nchi, kwa kuwa watu hao hawawezi kufanya maamuzi sahihi na kwa wakati sahihi.

Amempongeza Rais John Magufuli kwa kuhamasisha uanzishaji wa viwanda nchini na kuwa ni wajibu sasa kwa viwanda hivyo kujitathmini aina ya bidhaa za vyakula zinazozalishwa bila kuathili ubora wa vyakula vya asili kwa walaji.

Kwa upande wake Joanita Mutayoba, ambaye ni msomi na mjasiriamali, alisema ameanzisha mradi wa kutengeneza vyakula lishe vya mazao yanatokana na kilimo hai kwa ajili ya kujikimu kimaisha.

Alisema uamuzi wa kuanzisha kiwanda kidogo ambacho kinazalisha bidhaa kwa ajili ya walaji, kina lenga kuwajengea msukumo watu mbalimbali kuwa na utamaduni wa kula vyakula vya asili.



## 'Hospitali ya Mnazi Mmoja imezidiwa'

**Na Rahma Suleiman, ZANZIBAR**

SERIKALI ya Zanzibar imesema mradi wa ujenzi wa hospitali ya rufani na kituo cha utafiti wa maradhi mbalimbali, utafanyika kama ilivyopangwa.

Waziri wa Nchi, Ofisi ya Rais, Issa Haji Ussi, aliyasema hayo jana alipotoa ufafanuzi kuhusu utekelezaji wa mradi huo ambao ni sehemu ya utekelezaji wa ilani ya Chama Cha Mapinduzi (CCM).

Alisema nia ya Serikali ya Mapinduzi ya Zanzibar ni kujenga hospitali kubwa ya rufani ambayo itatoa huduma kwa wananchi wa Zanzibar.

Ussi alisema hospitali iliyopo sasa ya Mnazi Mmoja imezidiwa na wingi wa watu wanaohitaji huduma za afya, hivyo serikali iliona busara kujenga hospitali nyingine ya kisasa yenye hadhi ya rufani.

"Mheshimiwa Spika, nia ya kujenga hospitali ya kisasa ya rufani huko Binguni Wilaya ya Kati Unguja ipo palepale, tutajenga hospitali hiyo ambayo ni sehemu ya utekelezaji wa ilani ya uchaguzi ya CCM 2015-2020," alisema.

Alisema serikali pia inaendelea na mchakato wa ujenzi wa maabara ya kuchunguza maradhi ya binadamu ambayo yamekuwa yakisababisha vifo kwa wananchi wengi.

Waziri huyo alisema huo ni uamuzi uliochukuliwa na Rais wa Zanzibar, Dk. Ali Mohamed Shein, kwa lengo la kuhakikisha vipimo vya magonjwa hayo unafanyika nchini na siyo kupeleka sampuli nje ya nchi.

"Mheshimiwa Spika, mchakato wa ujenzi wa maabara ya kisasa ya kuchunguza maradhi ya binadamu unaendelea huko Binguni Wilaya ya kati. Maabara hiyo itapunguza na kuondosha tatizo la kusafirisha sampuli na kupeleka nje ya nchi," alisema.

Hivi karibuni, Rais Shein alitembelea eneo unakotarajiwa kutekelezwa mradi huo wa ujenzi wa maabara ya kisasa ya uchunguzi wa maradhi ya binadamu na kuitaka Wizara ya Fedha kusimamia mradi huo kwa kuwa fedha zipo.

# Rais Shein aagiza maofisa wadhamini kukabili maafa

**Na Rahma Suleiman, ZANZIBAR**

RAIS wa Zanzibar na Mwenyekiti wa Baraza la Mapinduzi, Dk. Ali Mohamed Shein, amewataka maofisa wadhamini kisiwani Pemba kufanya kazi ya kukabiliana na maafa kwenye maeneo ambayo wananchi wameathirika kwa kuwa kazi hiyo haina ofisa maalum.

Aliyasema hayo Ikulu ndogo ya Chake Chake, Mkoa wa Kusini Pemba, alipofanya mazungumzo na maofisa wadhamini wa wizara za Serikali ya Zanzibar wanaofanya kazi zao Pemba wakati wa ziara yake ya siku tatu kisiwani humo.

Rais Shein aliwataka viongozi hao kuzifanyia haraka tathmini za maafa kwa kila wilaya yakiwamo maeneo ya vijijini, ili kujua nani anatakiwa kusaidiwa na shughuli hizo zifanyike ipasavyo na kwa muda mwafaka.

Aliwataka viongozi hao kuwa mstari wa mbele katika kushirikiana na Kamisheni ya Kukabiliana na Maafa Zanzibar, ikiwa ni pamoja na kupambana na maradhi yanayosababishwa na virusi vya corona.

Dk. Shein aliwapongeza viongozi hao kwa kufanya kazi nzuri ya kupambana na maradhi yanayosababishwa na virusi vya corona kwa kushirikiana na Kamisheni ya Kukabiliana na Maafa Zanzibar na kusisitiza kuwa hilo ni jukumu la sekta zote za serikali.

Alibainisha kuwa, jukumu la kupambana na maradhi yanayosababishwa na virusi vya corona si la Wizara ya Afya pekee, bali ni la taasisi zote huku akiwapongeza viongozi wa Pemba kwa hatua wanazochukua kukabiliana na maradhi hayo.

Akizungumzia maafa yaliyosababishwa na mvua inayoendelea kunyesha, Rais Shein alisema mvua ni neema, lakini kuzidi kwake kiwango ndiko kulikopelekea maafa hayo na kuanguka kwa nyumba za wananchi.

Dk. Shein aliwataka maofisa wadhamini kutokaa ofisini, badala yake waende kwenye maeneo yao ya kazi kwa maslahi ya wananchi na serikali kwa jumla.



Waziri wa Nchi Ofisi ya Rais Utumishi wa Umma na Utawala Bora, Zanzibar, Haroun Ali Suleiman (kushoto), akibadilishana mawazo na Waziri wa Katiba na Sheria, Khamis Juma Maalim, nje ya ukumbi wa Baraza la Wawakilishi Zanzibar, juzi. **PICHA: RAHMA SULEIMAN**

# Ataka elimu kudhibiti corona

**Na Mwandishi Wetu, UNGUJA**

TAASISI za kijamii za kitaifa na kimataifa zina wajibu kuungana na serikali kutoa elimu kwa jamii jinsi taifa linavyoweza kufanikiwa kuvuka vyema kwenye mapambano dhidi ya virusi vya corona.

Kauli hiyo ilitolewa jana na Katibu Mkuu Ofisi ya Makamu wa Pili wa Rais wa Zanzibar, Shaaban Seif Mohamed, alipopokea mchango wa Sh. milioni 8.4, zilizowekwa kwenye akaunti ya Mfuko wa Corona zilizotolewa na wanachama wa Chama Kikuu cha Ushirika cha Kuweka na Kukopa (ZASCU) ofisini kwake Vuga mjini Zanzibar.

Shaaban alisema juhudi zinazochukuliwa na viongozi wakuu wa serikali zote mbili katika kukabiliana na janga la corona, hazina budi kuungwa mkono na wananchi kwa kuzingatia umuhimu wa kufanya kazi kwa bidii ili taifa lisonge mbele kiuchumi na maendeleo.

Alisema ugonjwa corona bado upo na unamgusa moja kwa moja kila mwanajamii, lakini kuchapa kazi ni wajibu kwa kila mwananchi katika sekta ya umma na hata zile za ujasiriamali.

Katibu Mkuu huyo aliwashukuru wanachama na viongozi wa chama hicho kwa wazo lao la kusaidia nguvu za serikali, akisisitiza kuwa taasisi nyingine zinakaribishwa kuchangia mfuko wa corona nchini.

Akitoa maelezo ya taasisi hiyo ya biashara kuamua kuchangia harakati za mapambano dhidi ya corona, Mwenyekiti wa Chama Kikuu cha Ushirika cha Kuweka na Kukopa, Rajab Haji Dawa, alisema janga la corona linawagusa moja kwa moja kwa vile asilimia kubwa ya wanachama wao ni wafanyabiashara wanaozunguka sehemu tofauti ndani na nje ya nchi.

Dawa alisema wanaushirika hao walihamasishana na kufikia hatua ya kuwagawia barakoa wananchi katika maeneo mbalimbali nchini, na pale serikali kuu ilipofungua milango ya michango, ndipo walipokuja la wazo la kuwasilisha mchango wao huo wa fedha.

Mkurugenzi wa Vyama vya Ushirika Zanzibar, Khamis Daudi Simba, alisema kanuni ya saba ya kimataifa ya vyama vya ushirika inavitaka vyama au vikundi vya ushirika kujali ustawi wa jamii unaovizunguka.

Daudi alisema uamuzi wa wanachama wa Chama Kikuu cha Ushirika cha Kuweka na Kukopa Zanzibar, unapaswa kupongezwa kwa vile umezingatia kanuni hiyo hasa kipindi hichi ambacho jamii imekumbwa na maradhi yanayosababishwa na virusi vya corona.

# MATANGAZO MCHANGANYIKO

*NIPASHE NI JIBU LAKO*

NJOO UTANGAZE NASI

KWA BEI NAFUU SANA

Tutumie E-mail: advertise@guardian.co.tz, au piga simu: 0782253676

**IN THE UNITED REPUBLIC OF TANZANIA**
**IN THE DISTRICT COURTOF DODOMA**
**AT DODOMA**
**PROBATE AND ADMINISTRATION CAUSE NO 29 OF 2020**
**In the Matter of the Estate of the Late Daudi Masiyanga Malanjiza**
**And**
**In the Matter of Application for Letters of Administration By Charles Daudi Malanjiza**

**GENERAL CITATION**

ALL PERSONS to have any interest in the estate of the above- named deceased are hereby cited to come and see the proceedings if they think fit before the grant of probate(or letters of Administration) is made to the above named Petitioner.

Objections to the grant should be filled on or before the 10 Day of JUNE 2020

The will of the said deceased is deposited and open for inspection at the Court.

Date at Dodoma this23rdday ofApril, 2020.

**KUPOTELEWA NA KADI YA GARI**

**JOSEPH HANDILO BUNDALA** anatangaza kupotelewa na kadi ya gari aina ya TOYOTA Hiace yenye namba za usajili T 622 CPF. Chassis No. KDH2000034403, EngineNo. 2KD1390993.

Yeyote atakayeiona atoe taarifa kituo cha polisi.

Taarifa ya polisi: KNG/RB/847/2017.

JAMHURI YA MUUNGANO WA TANZANIA
MAHAKAMA

USIMAMIZI WA MIRATHI (S.M.M.1984 NYONGEZA) YA 5 KANUNI YA 2
Katika mahakama ya mwanzo:
MJINI-MOROGORO
**Usimamizi wa mirathi No;119/2020**

Ombi la **YAHYA KITWANA SALUM** Kuteuliwa msimamizi wa mirathi marehemu **ZAWADI YAHYA MBEGU.**

Watu wote wanaodai kuwa na uhusiano wowote na mirathi ya marehemu kuwa wanaarikwa kuja na kuudhuria shaurini mnamo tarehe 10/06/2020 kabla ya muombaji hajateuliwa kuwa msimamizi wa mirathi hiyo.Wosia ya marehemu huyo upo mahakamani waweza kukaguliwa tarehe 13/05/2020.

*Kwa Habari*

*Motomoto*

*usikose Gazeti lako la*

**Kwa Habari Motomoto**

usikose Gazeti lako

la Nipashe kila siku

Tupigie

0782253676

Nipashe
www.ippmedia.com MWANGA WA JAMII

TAHADHARI: Wasomaji wanatakiwa kuuliza na kuchukua ushauri sahihi kabla ya kutuma fedha, au kuingia katika gharama yoyote kati yake na mtangazaji THE GUARDIAN LIMITED hawatahusika kwa malipo au manunuzi yoyote kati ya muuzaji na mnunuaji kwa matangazo yaliyochapishwa katika gazeti hili.

# TANGAZO

EXIM AT WORK TODAY | FOR TOMORROW

## "EXIM AT WORK TODAY, FOR TOMORROW"

EXIM AT WORK TODAY | FOR TOMORROW

**EXIM BANK (TANZANIA) UONESHAJI WA TAARIFA ZA FEDHA KWA UMMA ZILIZOKAGULIWA**
**Imetolewa chini ya kanuni ya 7 na ya 8 ya kanuni za Mabenki na Taasisi za Fedha (Uoneshaji) ya Mwaka 2014.**

Amana za wateja
@TZS 1.3 Trilioni

Jumla ya Mali
@ Trilioni 1.8

Matawi
@ 48

### WARAKA MIZANIA KWA TAREHE 31.12.2019 (KIASI KWA SHILINGI MILIONI)

| | | KUNDI MWAKA WA SASA 31.12.2019 | KUNDI MWAKA ULIOPITA 31.12.2018 | KAMPUNI MWAKA WA SASA 31.12.2019 | KAMPUNI MWAKA ULIOPITA 31.12.2018 |
|---|---|---|---|---|---|
| A | MALI | | | | |
| 1 | Fedha Taslimu | 42,243 | 35,526 | 24,393 | 21,561 |
| 2 | Salio Katika Benki Kuu ya Tanzania | 136,401 | 143,709 | 67,683 | 79,596 |
| 3 | Uwekezaji Katika Amana za Serikali | 244,827 | 234,779 | 241,033 | 220,110 |
| 4 | Salio Katika Benki Nyingine na Taasisi za Fedha | 70,955 | 31,913 | 31,796 | 47,277 |
| 5 | Hundi na Miamala ya Kushughulikiwa | 3,692 | 7,365 | 1,953 | 1,586 |
| 6 | Miamala Isiyoshughulikiwa Baina ya Matawi | - | - | - | - |
| 7 | Bili Zilizoafikiwa | - | - | - | - |
| 8 | Dhima za Wateja Zilizokubalika | - | - | - | - |
| 9 | Mikopo Iliyotolewa kwa Benki Nyingine | 158,631 | 121,496 | 111,051 | 45,575 |
| 10 | Uwekezaji Katika Amana Nyigine | 30,583 | 978 | 7,797 | 7,648 |
| 11 | Mikopo Halisi Iliyopo | 953,374 | 877,073 | 708,745 | 659,870 |
| 12 | Mali nyingine | 44,348 | 45,324 | 38,808 | 41,074 |
| 13 | Uwekezaji katika Hisa | 2,529 | 1,722 | 36,253 | 33,154 |
| 14 | Akaunti za udhamini | - | - | - | - |
| 15 | Mali Zisizohamishika, Mitambo na Vifaa | 81,414 | 47,682 | 60,090 | 36,696 |
| 16 | Mali isiyo ya sasa yanayotumiwa | 16,907 | 16,797 | 15,949 | 15,728 |
| 17 | **JUMLA YA MALI** | **1,785,904** | **1,564,365** | **1,345,551** | **1,209,875** |
| B | DHIMA | | | | |
| 18 | Amana za Benki na Taasisi za Fedha | 98,993 | 77,296 | 273,720 | 255,814 |
| 19 | Amana za Wateja | 1,298,177 | 1,175,831 | 721,308 | 670,049 |
| 20 | Dhamana ya Malipo kwa Fedha Taslimu | 8,486 | 5,032 | 6,852 | 3,774 |
| 21 | Amana Maalumu | - | - | - | - |
| 22 | Maagizo ya Malipo/Fedha za Kuhamisha | 282 | 230 | 282 | 230 |
| 23 | Hundi na Hawala za Kibenk Zilitolewa | 2,843 | 2,836 | 1,576 | 1,541 |
| 24 | Limbikizo la Kodi na Gharama Zitakazolipwa | 4,941 | 5,271 | 4,160 | 4,930 |
| 25 | Dhima la Tozo kwa Ajili ya Usuluhishi Baina ya benki | - | - | - | - |
| 26 | Miamala Isiyoshughulikiwa Baina ya Matawi | - | - | - | - |
| 27 | Mapato yaliyoingia ya Kipindi Kijacho na Tozo | 9,365 | 1,307 | 8,851 | 1,307 |
| 28 | Dhima Nyingine | 60,468 | 29,206 | 42,498 | 12,604 |
| 29 | Madeni | 144,220 | 100,397 | 144,220 | 100,397 |
| 30 | **JUMLA YA DHIMA** | **1,627,775** | **1,397,406** | **1,203,467** | **1,050,646** |
| 31 | **MALI/(DHIMA) HALISI (16 kutoa 29)** | **158,129** | **166,958** | **142,084** | **159,229** |
| C | FEDHA ZA WANAHISA | | | | |
| 32 | Mtaji wa Hisa Uliolipwa | 12,900 | 12,900 | 12,900 | 12,900 |
| 33 | Akiba ya Mtaji | 45,574 | 13,903 | 37,996 | 10,877 |
| 34 | Mapato Yaliyobakizwa | 103,705 | 144,967 | 108,957 | 149,447 |
| 35 | Faida (Hasara) ya Kipindi Husika | (14,993) | (15,779) | (17,769) | (13,995) |
| 36 | Akaunti Nyingine za Mtaji | - | - | - | - |
| 37 | Stahiki ya Wenyehisa Chache | 10,946 | 10,967 | - | - |
| 38 | **JUMLA YA FEDHA ZA WANAHISA** | **158,129** | **166,958** | **142,084** | **159,229** |
| 39 | Dhima Zisizo Dhahiri | 226,753 | 179,954 | 192,464 | 121,314 |
| 40 | Mikopo Chechefu | 199,022 | 110,007 | 169,393 | 91,341 |
| 41 | Tengo kwa Ajili ya Mikopo Chechefu | 78,457 | 83,537 | 57,825 | 71,095 |
| 42 | Mali Nyingine Chechefu | 2,914 | 8,235 | 2,914 | 8,235 |
| D | BAADHI YA VIASHIRIO VYA HALI YA KIFEDHA | | | | |
| | Uwiano wa Fedha za Wanahisa na Jumla ya Mali | 8.85% | 10.67% | 10.56% | 13.16% |
| | Uwiano wa Mikopo Chechefu na Jumla ya Mikopo Ghafi | 22.66% | 12.52% | 22.06% | 12.49% |
| | Uwiano wa Mikopo Ghafi na Jumla ya Amana | 75.56% | 75.56% | 77.16% | 78.18% |
| | Uwiano wa Mikopo Halisi na Jumla ya Mali Halisi | 53.37% | 56.07% | 52.67% | 54.54% |
| | Uwiano wa Mali Zinazozalisha na Jumla ya Mali | 81.79% | 81.05% | 84.47% | 83.78% |
| | Ongezeko la Amana | 11.49% | 1.58% | 7.47% | 0.03% |
| | Ongezeko la Mali | 14.18% | -2.45% | 11.22% | -4.37% |

### TAARIFA YA MAPATO NA MATUMIZI KWA MWAKA UNAOISHIA 31.12.2019 (KIASI KWA SHILINGI MILIONI)

| | | KUNDI MWAKA WA SASA 31.12.2019 | KUNDI MWAKA ULIOPITA 31.12.2018 | KAMPUNI MWAKA WA SASA 31.12.2019 | KAMPUNI MWAKA ULIOPITA 31.12.2018 |
|---|---|---|---|---|---|
| 1 | Mapato ya Riba | 130,794 | 132,770 | 102,552 | 108,595 |
| 2 | Gharama za Riba | (36,527) | (31,255) | (33,600) | (29,735) |
| 3 | Mapato Halisi ya Riba (1kutoa 2) | **94,267** | **101,515** | **68,952** | **78,860** |
| 4 | Madeni Viza Yaliyofutwa | - | - | - | - |
| 5 | Punguzo/Ongezeko la tengo katika Mikopo | (39,994) | (20,508) | (29,254) | (16,160) |
| 6 | **Mapato Yasiyo ya Riba:** | **57,201** | **50,626** | **34,442** | **37,249** |
| | 6.1 Faida /(Hasara) Zitokanazo na Miamala ya Fedha za Kigeni | 13,807 | 12,257 | 8,599 | 6,572 |
| | 6.2 Ada na Kamisheni | 35,817 | 34,977 | 20,384 | 23,849 |
| | 6.3 Gawio | 21 | 21 | 21 | 21 |
| | 6.4 Mapato Mengine | 7,556 | 3,371 | 5,438 | 6,807 |
| 7 | **Gharama Zisizo za Riba:** | **(119,852)** | **(126,911)** | **(88,666)** | **(94,913)** |
| | 7.1 Mishahara na Mafao | (53,058) | (51,997) | (35,578) | (35,339) |
| | 7.2 Ada na Kamisheni | (174) | (133) | (161) | (85) |
| | 7.3 Gharama Nyingine | (66,620) | (74,782) | (52,927) | (59,490) |
| 8 | **Faida /(Hasara) ya Uendeshaji** | **(8,378)** | **4,721** | **(14,526)** | **5,035** |
| 9 | Tengo la Kodi ya Mapato | (6,615) | (20,500) | (3,243) | (19,031) |
| 10 | **Faida / (Hasara) Halisi Baada ya Kodi ya Mapato** | **(14,993)** | **(15,779)** | **(17,769)** | **(13,996)** |
| 11 | Idadi ya Waajiriwa | 1,000 | 972 | 688 | 704 |
| 12 | Mapato kwa Hisa | (1,162) | (1,223) | (1,377) | (1,085) |
| 13 | **Idadi ya Matawi** | **48** | **46** | **33** | **33** |
| | **BAADHI YA VIASHIRIO VYA HALI YA KIFEDHA** | | | | |
| (I) | Uwiano wa Faida Kabla ya Kodi na Wastani wa Mali | -1% | -1% | -1% | -1% |
| (II) | Uwiano wa Faida baada ya Kodi na Wastani wa Fedha za Wanahisa | -9% | -6% | -12% | -6% |
| (III) | Uwiano wa Matumizi Yasiyo ya Riba na Mapato Ghafi | 79% | 83% | 86% | 82% |
| (IV) | Uwiano wa Mapato Halisi ya Riba na Wastani wa Mali Zinazozalisha | 7% | 8% | 7% | 7% |

### TAARIFA YA MTIRIRIKO WA FEDHA KWA MWAKA ULIOISHIA 31.12.2019 (KIASI KWA SHILINGI MILIONI)

| | | KUNDI MWAKA WA SASA 31.12.2019 | KUNDI MWAKA ULIOPITA 31.12.2018 | KAMPUNI MWAKA WA SASA 31.12.2019 | KAMPUNI MWAKA ULIOPITA 31.12.2018 |
|---|---|---|---|---|---|
| I | **Mtiririko wa Fedha Kutokana na Shughuli za Uendeshaji:** | | | | |
| | Mapato/(Hasara) Halisi | **(8,378)** | **4,721** | **(14,526)** | **5,035** |
| | Marekebisho kwa Ajili ya: | | | | |
| | Hasara Katika Mali | 68,264 | 35,800 | 49,708 | 34,004 |
| | Badiliko Halisi Katika Mikopo | (115,092) | (46,216) | (67,322) | (37,250) |
| | Faida/Hasara Kwenye Mauzo ya Mali | - | - | - | - |
| | Mabadiliko Halisi Katika Amana | 140,533 | 19,541 | 66,710 | 305 |
| | Mabadiliko Halisi Katika Amana za Muda Mfupi Zilizoafikiwa | - | - | - | - |
| | Mabadiliko Halisi Katika Dhima Nyingine | 10,712 | (2,402) | 11,700 | (9,002) |
| | Mabadiliko Halisi Katika Mali Nyingine | (508) | 5,565 | (700) | 1,126 |
| | Non-current assets held for sale | (110) | 1,484 | (221) | 466 |
| | Kodi Iliyolipwa | (6,570) | (4,934) | (4,731) | (2,495) |
| | Mengineyo (bainisha) | (23,776) | 36,353 | (27,274) | 47,601 |
| | **Fedha Halisi zilizotolewa (zilizotumika) kwa shughuli za uendeshaji** | **65,075** | **49,912** | **13,344** | **39,790** |
| II | **Mtiririko wa Fedha Kutokana na Shughuli za Uwekezaji:** | | | | |
| | **Gawio Lililopokewa** | **21** | **21** | **21** | **21** |
| | Ununuzi wa Mali za Kudumu | (11,208) | (9,441) | (5,351) | (4,476) |
| | Mapato Kutokana na Mauzo ya Mali za Kudumu | - | - | 7 | - |
| | Ununuzi wa Amana Zisizoshughulikiwa na Mawakala | - | - | - | - |
| | Mapato Kutokana na Mauzo ya Amana Zisizoshughulikiwa na Mawakala | - | - | - | - |
| | Mengineyo (Uwekazaji katika hisa) | (3,300) | (765) | (7,353) | (765) |
| | Fedha Halisi Zilizotolewa (zilizotumika) kwa Shughuli za Uwekezaji | (14,487) | (10,185) | (12,676) | (5,220) |
| III | **Mtiririko wa Fedha Kutokana na Shughuli za Kifedha:** | | | | |
| | **Ulipaji wa Madeni ya Muda Mrefu** | **(26,932)** | **(30,848)** | **(26,932)** | **(30,848)** |
| | Mapato Kutokana na Utoaji wa Madeni ya Muda Mrefu | 62,159 | 23,000 | 62,159 | 23,000 |
| | Mapato Kutokana na Utoaji wa Mtaji wa Hisa | 2,863 | - | - | - |
| | Gawio Lililolipwa kwa Fedha Taslimu | - | - | - | - |
| | Mabadiliko Halisi Katika Madeni Mengine | - | - | - | - |
| | Mengineyo (bainisha) | - | - | - | - |
| | Fedha Halisi Zilizotolewa (zilizotumika) kwa Shughuli za Kifedha | 38,090 | (7,848) | 35,227 | (7,848) |
| IV | **Fedha Taslimu na Mali Zinazofanana na Fedha Taslimu:** | | | | |
| | **Ongezeko / Punguzo Halisi Katika Fedha taslimu na Mali Zinazofanana na Fedha Taslimu** | **88,678** | **31,879** | **35,895** | **26,722** |
| | Fedha na Mali Zinazofanana na Fedha Taslimu Mwanzoni mwa Robo Mwaka/Mwaka | **296,452** | **264,542** | **198,704** | **171,953** |
| | Fedha na Mali Zinazofanana na Fedha Taslimu Mwishoni mwa Robo Mwaka/Mwaka | **385,130** | **296,452** | **234,599** | **198,704** |

### TAARIFA YA MABADILIKO YA MTAJI KWA KIPINDI KINACHOISHIA 31.12.2019 (KIASI KWA SHILINGI MILIONI)

| KAMPUNI | Mtaji wa Hisa | Malipo juu ya bei ya hisa | Mapato Yaliyobakizwa | Ziada ya Kisheria | Tengo la Ziada ya Jumla | "Mengineyo (bainisha)" | Jumla |
|---|---|---|---|---|---|---|---|
| **Mwaka wa sasa** | | | | | | | |
| **Salio jipya la mwanzo wa mwaka 01.01.2019** | **12,900** | - | **135,452** | **4,488** | **6,402** | **(13)** | **159,229** |
| Faida / (Hasara) Halisi Baada ya Kodi ya Mapato | - | - | (17,769) | - | - | - | (17,769) |
| Mapato mengine yaliyojumuishwa | - | - | - | - | - | 624 | 624 |
| Miamala na wanahisa | - | - | - | - | - | - | - |
| Gawio lililolipwa | - | - | - | - | - | - | - |
| Ziada ya Kisheria | - | - | (32,897) | 32,897 | - | - | - |
| Tengo la Ziada ya Jumla | - | - | 6,402 | - | (6,402) | - | - |
| Mengineyo | - | - | - | - | - | - | - |
| **Salio la mwisho wa mwaka** | **12,900** | - | **91,187** | **37,385** | - | **611** | **142,084** |
| **Mwaka Uliopita** | | | | | | | |
| **Salio la mwanzo wa mwaka** | **12,900** | - | **158,809** | **35,486** | **6,363** | **54** | **213,612** |
| Mabadiliko ya mwanzo ya IFRS 9 | - | - | (40,321) | - | - | (119) | (40,440) |
| Marekebisho mengine | - | - | 23,705 | (23,705) | - | - | - |
| **Salio jipya la mwanzo wa mwaka 01.01.2018** | **12,900** | - | **142,193** | **11,781** | **6,363** | **(65)** | **173,172** |
| Faida / (Hasara) Halisi Baada ya Kodi ya Mapato | - | - | (13,995) | - | - | - | (13,995) |
| Mapato mengine yaliyojumuishwa | - | - | - | - | - | 52 | 52 |
| Miamala na wanahisa | - | - | - | - | - | - | - |
| Gawio lililolipwa | - | - | - | - | - | - | - |
| Ziada ya Kisheria | - | - | 7,293 | (7,293) | - | - | - |
| Tengo la Ziada ya Jumla | - | - | (39) | - | 39 | - | - |
| Mengineyo | - | - | - | - | - | - | - |
| Salio la mwisho wa mwaka | 12,900 | - | 135,452 | 4,488 | 6,402 | (13) | 159,229 |

| KUNDI | Mtaji wa Hisa | Malipo juu ya bei ya hisa | Mapato Yali-yobakizwa | Ziada ya Kisheria | Tengo la Ziada ya Jumla | "Mengineyo (bainisha)" | Jumla |
|---|---|---|---|---|---|---|---|
| **Mwaka wa sasa** | | | | | | | |
| **Salio jipya la mwanzo wa mwaka 01.01.2019** | **12,900** | - | **129,227** | **8,865** | **6,290** | **9,167** | **166,449** |
| Faida / (Hasara) Halisi Baada ya Kodi ya Mapato | - | - | (13,473) | - | - | (1,179) | (14,993) |
| Mapato mengine yaliyojumuishwa | - | - | - | - | 3,812 | (3) | 3,809 |
| Miamala na wanahisa | - | - | - | - | - | 2,863 | 2,863 |
| Gawio lililolipwa | - | - | - | - | - | - | - |
| Ziada ya Kisheria | - | - | (32,897) | 32,897 | - | - | - |
| Tengo la Ziada ya Jumla | - | - | 6,196 | - | (6,290) | 95 | - |
| Mengineyo | - | - | - | - | - | - | - |
| **Salio la mwisho wa mwaka** | **12,900** | - | **88,712** | **41,762** | **3,812** | **10,943** | **158,129** |
| **Mwaka Uliopita** | | | | | | | |
| **Salio la mwanzo wa mwaka** | **12,900** | - | **152,685** | **46,457** | **6,447** | **12,965** | **231,454** |
| Mabadiliko ya mwanzo ya IFRS 9 | - | - | (47,668) | (119) | - | (828) | (48,615) |
| Marekebisho mengine | - | - | 23,594 | (23,437) | (157) | - | - |
| **Salio jipya la mwanzo wa mwaka 01.01.2018** | **12,900** | - | **128,611** | **22,901** | **6,290** | **12,137** | **182,839** |
| Faida / (Hasara) Halisi Baada ya Kodi ya Mapato | - | - | (12,380) | - | - | (3,399) | (15,779) |
| Mapato mengine yaliyojumuishwa | - | - | - | - | - | (562) | (562) |
| Miamala na wanahisa | - | - | - | - | - | (49) | (49) |
| Gawio lililolipwa | - | - | - | - | - | - | - |
| Ziada ya Kisheria | - | - | 12,148 | (14,036) | - | 1,888 | - |
| Tengo la Ziada ya Jumla | - | - | 848 | - | - | (848) | - |
| Mengineyo | - | - | - | - | - | - | - |
| **Salio la mwisho wa mwaka** | **12,900** | - | **129,227** | **8,865** | **6,290** | **9,167** | **166,449** |

The above extracts are from the Financial Statements of the bank for the year ended December 31, 2019 which have been prepared in accordance with International Financial Reporting Standards (IFRS). The Financial Statements were audited by Deloitte CPAs with clean audit report. The financial Statements were approved by the board of directors and signed on its behalf by:

| JINA NA CHEO | SAINI | TAREHE |
|---|---|---|
| JUMA MWAPACHU<br>**KAIMU MWENYEKITI WA BODI** | ………………………………….. | **14.05.2020** |

Kwa maelezo zaidi piga simu 080 078 0111 au tembelea visit www.eximbank.co.tz

EXIM BANK
Innovation is life

# CEBALLOS: NITAFANIKIWA TU REAL MADRID



**MADRID,** Hispania

DANI Ceballos bado ana matumaini ya kupata mafanikio katika Klabu ya Real Madrid licha ya kucheza kwa mkopo pale Arsenal.

Ceballos mwenye umri wa miaka 23 alijiunga na klabu hiyo ya Ligi Kuu England kwa mkopo wa muda mrefu, na amecheza mechi 24 kabla ya msimu kusimamishwa kutokana na mlipuko wa virusi vya corona.

Raia huyo wa Hispania ambaye ameichezea timu yake ya taifa mechi tisa mkataba wake pale Madrid unamalizika mwaka 2023 na anataka kuendelea kupata nafasi ya kuwachezea miamba hao wa LaLiga.

"Ninacheza na nina mkataba na Real Madrid," amesema Ceballos akiliambia gazeti la Deportes Cuatro, Jumatano.

"Nina umri wa miaka 23. Najihisi kama mchezaji niliyekamilika na nimejiandaa kwa changamoto yoyote itakayokuja mbele yangu."

Ceballos alijiunga na Madrid kutoka Real Betis kwa ada iliyoripotiwa kuwa euro milioni 18 Julai mwaka 2017.

# Ferdinand azungumzia hatima ya Kane Spurs

**LONDON,** England

KLABU ya Tottenham inatakiwa kutimiza malengo ya Harry Kane au vinginevyo mshambuliaji huyo ataondoka na kwenda kutafuta mafanikio ya kubeba taji sehemu nyingine, kwa mujibu wa Les Ferdinand.

Nahodha Kane hajashinda taji lolote akiwa na Spurs licha ya kuwa na uwezo mkubwa wa kufunga mabao, wakifungwa kwenye fainali ya EFL mwaka 2015 na Chelsea, kabla ya kupoteza kwenye fainali ya Ligi ya Mabingwa Ulaya dhidi ya Liverpool jijini Madrid mwaka jana.

Na hiyo ndio sababu klabu hiyo ikamtimua kocha wake, Mauricio Pochettino na nafasi yake ikachukuliwa na Jose Mourinho.

Hata hivyo, raia huyo wa Ureno ameshindwa kuwa na mafanikio makubwa katika klabu hiyo tangu achukue mikoba.

Tayari wameshatolewa kwenye mashindano ya Ulaya na RB Leipzig, na sasa Tottenham walichobakia ni kupigania kumaliza nafasi ya nne kwenye msimamo wa Ligi ili wafuzu kucheza Ligi ya Mabingwa Ulaya msimu ujao.

Kane, ambaye amekuwa akihusishwa na kuwania na klabu kadhaa zikiwamo Manchester United pamoja na Real Madrid, alikubali mwezi uliopita kwamba hatabakia pale Tottenham "ilimradi tu", na kuibua shaka juu ya majaliwa yake ya baadaye.

Na sasa mshambuliaji wa zamani wa Spurs, Ferdinand anahofia waajiri wake hao wa zamani kama wanaweza kumbakisha mshambuliaji huyo kama hawatakuwa kwenye nafasi ya kutwaa mataji.

"Kama shabiki, sitaki Harry aende popote. Nataka abakie Tottenham na kumalizia kipindi chake cha uchezaji Tottenham, lakini tunatakiwa kuwa na mipango," amesema Ferdinand akiiambia Sky Sport.






# *Shevchenko ataka kurudi AC Milan*

**MILAN,** Italia

ANDRIY Shevchenko amethibitisha angependa siku moja kurudi AC Milan kama kocha mkuu wa klabu hiyo inayoshiriki Serie A.

Shevchenko mwenye umri wa miaka 43, amekuwa kocha wa Ukraine tangu mwaka 2016 ikiwa ni mara ya kwanza kuinoa timu ya wakubwa.

Fowadi huyo wa zamani wa AC Milan na Chelsea wakati wake wa uchezaji alishinda taji la Ligi Kuu Italia, Serie A, pamoja na la Ligi ya Mabingwa Ulaya pale kwenye dimba la San Siro. Shevchenko ana matumaini ya siku moja kurudi pale Milan - kama kocha wao mkuu.

"Milan siku zote ipo moyoni mwangu na siku moja nitakapoamua kubadilika, ningependa kuwanoa wao," amesema wakati wa mahojiano live kupitia Instagram.

Milan imekuwa ikisuasua katika misimu ya hivi karibuni, kwa mara ya mwisho ilishinda taji la Serie A, msimu wa 2010/11.

Walikuwa nafasi ya saba kwenye msimamo wakati msimu huu ulipositishwa kutokana na mlipuko wa virusi vya corona na Shevchenko ana matumaini Milan inaweza kuimarika wakati msimu utakaporudi.

# HAALAND AIPOTEZEA REAL MADRID



**DORTMUND,** Ujerumani

NYOTA wa Borussia Dortmund, Erling Haaland, amesisitiza yuko imara na timu yake licha ya uvumi kusambaa kwamba alikuwa akitakiwa na vigogo wa Hispania, Real Madrid.

Haaland mwenye umri wa miaka 19, amekuwa mmoja wa fowadi anayetajwa zaidi barani Ulaya baada ya kuwa na kiwango cha kuvutia pale Dortmund.

Mchezaji huyo wa kimataifa wa Norway aling'ara kule Salzburg kabla ya kujiunga na miamba hao wa Bundesliga, Januari, na amefunga mabao 12 katika mechi 11 alizoichezea Dortmund msimu huu.

Huku Madrid wakiwa wanahusishwa sana na uhamisho wa Haaland, kinda huyo amesema yeye alikuwa akiangalia zaidi kiwango chake na sio kusikiliza mambo mengine.

"Nilijikuta kwenye kiwango changu, sikuwa nawaza chochote," amesema akiiambia Sky Sport.

"Nafikiri zaidi kuhusu kazi yangu, kitu ambacho nakipenda zaidi. Akili yangu ndio ipo huku."

Haaland aliongeza: "Bila shaka yoyote nilianza vizuri hapa Dortmund. Najaribu kufanya kazi kwa nguvu ili kujiimarisha zaidi kila siku."

## Vieira: Arteta ameleta nguvu mpya Arsenal

**LONDON,** England

PATRICK Vieira amemsifia Mikel Arteta kwa kuleta mabadiliko Arsenal, akisema kocha huyo mkuu ameleta nguvu mpya ndani ya klabu hiyo.

Arteta amekuwa akisifiwa tangu alipoichukua timu hiyo Desemba mwaka jana, akiwa amepoteza mechi mbili tu kati ya 15 tangu akabidhiwe mikoba.

Nahodha wa zamani wa Arsenal, Vieira, ambaye alikuwa akihusishwa na mpango wa kupewa kazi hiyo, amesifia kazi ya Arteta pale kwenye dimba la Emirates.

"Wewe kama ni mshikabunduki, mara zote ni mshikabunduki tu, hivyo huwa nawaangalia muda wote, natazama mechi zao," amesema kocha huyo mkuu wa Nice katika mahojiano na Ian Wright.

"Kitu ambacho kinanifurahisha kwa Arteta kwamba amerudisha nguvu ya klabu na sasa inaonyesha wachezaji wanacheza kwa ajili ya klabu, na nafikiri hili ni jambo muhimu sana."

Vieira amekuwa kocha wa Nice tangu mwaka 2018, na alikuwa akihusishwa na mpango wa kurudi Arsenal baada ya kufukuzwa kwa Unai Emery mwaka jana.



## PSG kumbakisha Cavani



**PARIS,** Ufaransa

EDINSON Cavani ana matumaini miaka kadhaa imebakia ya kucheza soka, wakati uvumi ukiendelea kukua kuwa Paris Saint-Germain wanapigania kumbakisha mfungaji huyo bora wa wakati wote wa klabu hiyo.

Mchezaji huyo wa kimataifa wa Uruguay bado hana uhakika kuhusu majaliwa yake hapo PSG, huku mkataba wake pale Parc des Princes ukiwa unamalizika mwishoni mwa Juni.

Hata hivyo, upigaji wa kura uliondeshwa na gazeti la kila siku la L'Equipe la nchini Ufaransa, umeonyesha kwamba, mashabiki wengi wa klabu hiyo wanataka Cavani abaki.

Kati ya kura zilizopigwa, 46,592 ambayo ni sawa na asilimia 77 zinataka mchezaji huyo mwenye umri wa miaka 33 kubakishwa klabuni hapo.

Na Cavani ameliambia gazeti la PSG: "Kipindi changu cha uchezaji pengine kimebakiza miaka kadhaa ya kucheza.

"Nimezungumza sana na wachezaji wenzangu pamoja na maofisa wa klabu. Mara zote nimesema ningependa kuachana na soka kuliko soka kuniacha mimi."

Alisajiliwa akitokea Napoli mwaka 2013 na Cavani ndiye mfungaji aliyeweka rekodi ya kufunga mabao klabuni hapo, akiwa amefunga mabao 200.

# DONDOO ZA SOKA
## MAGAZETI YA ULAYA



# MARTINEZ AKARIBIA KUTUA BARCELONA

●●● Ni baada ya straika huyo kuitaka klabu yake isifanyie kazi ofa kutoka City, PSG na...

**MILAN,** Italia

STRAIKA Lautaro Martinez ameiambia Inter Milan kutopokea ofa yoyote itakayowasilishwa na Manchester City au Paris St-Germain na kufunguka moyo wake unajiandaa kujiunga na Barcelona, zimeandika taarifa mbalimbali nchini Hispania.

**Wakati straika huyo akiwa na furaha kuendelea kutumikia klabu hiyo ya San-Siro, uwezekano wa kuungana na mchezaji mwenzake wa Timu ya Taifa ya Argentina, Lionel Messi katika LaLiga unaoneka unaweza kukamilika, unasubiriwa uamuzi wa Barca kwenye kukamilisha mchakato huo.**

Kwa mujibu wa gazeti la Mundo Deportivo, linaandika vigogo hao wa Katalan wanatajwa kuwa na nafasi kubwa ya kumsajili nyota huyo mwenye umri wa miaka 22 baada ya Martinez kuiambia Inter kuifanyia kazi ofa itakayowasilishwa na klabu hiyo ya Nou Camp.

Huku tayari Barcelona ikipewa nafasi nzuri ya kumsajili straika huyo, lakini bado klabu hiyo mbili zitatakiwa kufikia makubaliano kuhusiana na dau, Inter imetaja thamani ya Martinez ni pauni milioni 97.

Barcelona inamwona Martinez kama nyota atakayechukua mikoba itakayoachwa na Luis Suarez ndani ya klabu hiyo, huku akihusishwa na tetesi za kuwindwa na klabu zinazoshiriki Ligi Kuu Marekani endapo ataamua kuhama.

Mabingwa hao wa Ligi Kuu Hispania wanajiandaa kutoa wachezaji ili kukamilisha mchakato wa kumsajili Martinez pamoja na fedha kwa lengo la kumnasa straika huyo.

Beki wa kulia, Nelson Semedo naye anatajwa huenda akawa sehemu ya usajili huo wa kumnasa Martinez wakati Arturo Vidal na Antoine Griezmann nao wanawezekana pia kuhusishwa kwenye mazungumzo ya kuuzwa.

Martinez amefunga mabao 16 katika mechi 31 alizoitumikia klabu yake msimu huu na akionyesha pia kiwango cha juu kwenye michezo ya Ligi ya Mabingwa Ulaya ambayo alifunga magoli matano katika michezo sita aliyocheza.

Mkataba wake na Inter Milan unatarajiwa kukamilika Juni, mwaka 2023 baada ya kutua klabuni hapo akitokea Racing Club katika kipindi cha majira ya joto mwaka 2018.

## ZISIKUPITE

### SANE AKARIBIA BAYERN

BAYERN Munich inajiandaa kuwasilisha ofa ya zaidi ya pauni milioni 50 ili kuhakikisha mchakato wa kumsajili winga wa Manchester City, Leroy Sane, ambaye anatarajia kumaliza mkataba wake wa kuitumikia klabu hiyo ya Ligi Kuu England mwishoni mwa msimu ujao. ***(Telegraph)***

### DEMBELE ANUKIA UNITED

MANCHESTER United inakaribia kumsajili straika wa Timu ya Taifa ya Ufaransa na Lyon, Moussa Dembele (23), ambaye anawindwa na Chelsea, thamani ya nyota huyo ni pauni milioni 61.8. ***(Todofichajes, via Express)***

### BELLINGHAM DIMBANI

MANCHESTER United inamtaka kiungo chipukizi, Jude Bellingham (16), kuhakikisha anapambana kupata namba katika kikosi cha kwanza endapo watakamilisha mchakato wa kumsajili akitokea Birmingham City katika kipindi cha majira ya joto. ***(Evening Standard)***

### CHELSEA, PSG ZAVUTANA

CHELSEA iko tayari kumuuza kiungo wake Mfaransa Tiemoue Bakayoko (25), kwa dau la pauni milioni 31, lakini Paris St-Germain haitaki kutoa zaidi ya pauni milioni 26.5 ili kumsajili mchezaji huyo. ***(Le10 Sport, via Star)***

### DEMBELE SOKONI

BARCELONA imetaja dau la kumuuza mshambuliaji wa Timu ya Taifa ya Ufaransa, Ousmane Dembele (22), kuwa ni pauni milioni 53. Barca ilimsajili nyota huyo kwa dau la pauni milioni 135.5. ***(Marca, via Star)***

### BARCA YAMTAKA FOYTH

BEKI wa Tottenham, Juan Foyth amepata ofa za kujiunga na klabu mbalimbali na Barcelona ikitajwa pia kumwania nyota huyo raia wa Argentina ambaye ana umri wa miaka 22. ***(Mirror)***

### WEST YAMFIKIRIA MURIQI

WEST Brom itachuana na Tottenham katika vita ya kuwania saini ya mshambuliaji wa Fenerbahce na Timu ya Taifa ya Kosovo, Vedat Muriqi (26), kama itafanikiwa kupanda daraja kucheza Ligi Kuu England msimu ujao. ***(Aksam, via Birmingham Mail)***

### SCIGLIO ANUKIA BARCA

BARCELONA imeanza mazungumzo na Juventus kwa ajili ya kumsajili beki wa Timu ya Taifa ya Italia, Mattia de Sciglio (27), anayeichezea klabu hiyo ya Serie A baada ya mchakato wa kunasa saini ya beki wa kulia wa Ureno, Nelson Semedo (26), kushindikana. ***(Marca)***

### BALLACK AMFUNDA KAI

NYOTA wa zamani wa Timu ya Taifa ya Ujerumani, Michael Ballack, amemtaka kiungo wa Bayer Leverkusen, Kai Havertz (20), ambaye anawindwa na Liverpool, Manchester United na Chelsea kubakia katika klabu yake. ***(Football London)***

### TRAORE AIOTA PSG

BEKI wa Rennes ambaye ni raia wa Mali, Hamari Traore (28), ameanza mazungumzo ya kujiunga na mabingwa wa Ligue 1, PSG na ameeleza kujiunga na timu hiyo ni moja ya ndoto zake. ***(goal.com)***

HABARI MICHEZO

## Azam yashauri maproo wasipungue

**Na Saada Akida**

MABINGWA watetezi wa mashindano ya Kombe la FA, Azam FC wameitaka serikali na Shirikisho la Soka Tanzania (TFF), kutopunguza idadi ya nyota wa kigeni wanaopaswa kusajiliwa na timu zinazoshiriki Ligi Kuu Bara.

Akizungumza na gazeti hili jijini Dar es Salaam jana, Ofisa Mtendaji Mkuu wa timu hiyo, Abdulkarim Amin 'Popat' alisema kwa upande wao idadi ya wachezaji wakigeni inatakiwa ibakie kama ilivyo sasa kwa sababu inachangia kuwapa changamoto nyota wazawa.

Popat alisema nyota hao wa kulipwa huongeza ushindani wa kuwania namba katika timu na hali hiyo huinua viwango vya wachezaji wa hapa nchini.

"Wachezaji hawa wageni wanachangia kuwapa kiu ya wao pia kutoka nje kwenda kujaribu bahati zao, pia inatusaidia kwenye mashindano ya kimataifa kwa klabu tunapoenda kukutana wachezaji wenye viwangu vya juu," alisema Popat.

Aliongeza bado klabu za Tanzania hazina uwezo kama zilivyo timu za Waarabu kwa kutumia wachezaji wengi wazawa.

Aliongeza maoni ya Azam hayawezi kufanana na klabu nyingine kwa sababu nyingi hazina uwezo wa kifedha wa kusajili hata wachezaji wa ndani inaowahitaji.

## Alliance kurejea Ligi Kuu kitofauti

**Na Shufaa Lyimo**

UONGOZI wa Alliance FC yenye maskani yake jijini Mwanza umesema wamejipanga kufanya mabadiliko katika mechi za Ligi Kuu Tanzania Bara mara ligi hiyo itakapotangazwa kurejea tena, imeelezwa.

Makamu mwenyekiti wa klabu hiyo, Stephano Nyaitati alisema hawatakubali kuona wanashuka daraja ingawa wanakiri hawakufanya vizuri msimu huu.

"Kuna baadhi ya michezo hatukufanya vizuri, kabla ligi haijasimama kutokana na ugonjwa wa corona, tunaendelea kupambana ili tusishuke daraja kirahisi," alisema Nyaitati.

Kiongozi huyo alisema tayari wameyafanyia kazi makosa ambayo yalijitokeza katika mechi zilizopita na katika kipindi hiki cha mapumziko, wamewapa mbinu mpya wachezaji wao kupitia njia ya video.

"Tunawasiliana na wachezaji wetu mara kwa mara kwa njia ya video huku tukiwasisitiza kujituma zaidi, hatutaki na hatutarajii kushuka daraja, tutapambana hadi dakika ya mwisho," alisema.

Aliongeza umoja na ushirikiano wa kikosi chao umeimarika kwa sababu wote wanafahamu timu iko kwenye nafasi mbaya na hawataki kurudia makosa yaliyopita.

# RAIS ZFF ASHTAKIWA SERIKALINI KWA UBABE

**Na Faustine Feliciane**

WAJUMBE sita wa Kamati ya Utendaji ya Shirikisho la Soka Zanzibar (ZFF), wameandika barua kwa Mrajisi wa Vyama vya Michezo visiwani humo kueleza kutokuwa na imani na Rais wa shirikisho hilo, Seif Kombo Pandu, imefahamika.

**Barua hiyo imeelezea kutokubaliana na baadhi ya uamuzi unaofanya na Pandu katika shughuli za uendeshaji wa shirikisho hilo.**

Kwa mujibu wa taarifa zilizopatikana, katika barua hiyo wameelezea kushangazwa na kitendo cha Pandu kutangaza kuitisha kikao cha kamati ya utendaji kwa kuhusisha baadhi ya wajumbe ambao si halali.

Mmoja wa wajumbe hao walioandika barua hiyo ambaye hakutaka jina lake kutajwa, alisema Pandu amekuwa akiliendesha shirikisho hilo bila kufuata taratibu na kanuni za ZFF.

"Kuna mambo mengi yanaendelea ambayo yanafanywa na kiongozi tu (Rais), bila baraka na makubaliano ya Kamati ya Utendaji, tumeandika barua kuelezea kutokuwa na imani naye," alisema mjumbe huyo.

Akizungumza na gazeti hili, Ofisa mmoja wa Ofisi ya Mrajisi, Mohammed Said Mwinyi, alithibitisha kupokea barua hiyo na kueleza wanaifanyia kazi.

Mwinyi alisema tayari ofisi yake inasisitiza kuwapo kwa mazungumzo ya amani kabla ya kuchukua hatua zinazostahili kwa kuangalia katiba ya ZFF.

"Ni kweli tumepokea barua yao ikielezea malalamiko yao juu ya Rais wa ZFF, tunafanyia kazi, lakini tueleze tu mambo kama haya hayapaswi kupelekwa kwenye vyombo vya habari. ZFF wana katiba inayoelezea namna ya kumaliza matatizo yao," alisema Mwinyi.

Aliongeza kwa kuwataka viongozi wa shirikisho hilo kufanya mazungumzo pale wanapoona mambo hayaendi sawa sawa na kuacha tabia ya kueleza migogoro yao nje ya shirikisho kwa sababu kwa kufanya hivyo, huleta ugumu katika kufanya usuluhishi.



Wachezaji wa Vijana FC ya Temeke jijini Dar es Salaam, Hashim Ibrahim (kulia) na Abdallah Hamad, wakiwania mpira katika mazoezi ya timu hiyo kwenye viwanja vya pembeni ya Uwanja wa Taifa hivi karibuni. **PICHA: JUMANNE JUMA**

# Hilika awaza kiatu cha dhahabu

**Na Hawa Abdallah,** ZANZIBAR

MSHAMBULIAJI wa Zimamoto, Ibrahim Hilika amesema malengo yake ni kuona anatwaa tuzo ya Mfungaji Bora katika msimu huu wa Ligi Kuu Zanzibar.

Akizungumza na gazeti hili jana, Hilika ambaye ana mabao 11 na katika orodha ya wafungaji yuko kwenye nafasi ya tatu alisema anaendelea kujiimarisha ili ndoto zake za kutwaa tuzo hiyo kwa mara ya tatu mfululizo iweze kutimia.

Hilika alisema anataka kuona 'kiu' yake ya kuweka rekodi kwenye Ligi Kuu Zanzibar inakamilika na sasa anafanya mazoezi kwa bidii, huku akisubiri taarifa ya kurejea kwa ligi hiyo ambayo bado imesimama kutokana na janga la corona.

"Ninafanya mazoezi kwa bidii kubwa ii malengo yangu ya kuwa mfungaji bora yatimie, nataka kujitengenezea rekodi nzuri, ninataka kuwa mshambuliaji mwenye historia ya kupachika magoli misimu mingi katika Ligi Kuu hapa nchini," alisema Hilika.

Aliongeza licha ya ushindani ulioko katika Ligi Kuu Zanzibar, bado washambuliaji wanapambana kutimiza malengo yao ya kucheza soka la kulipwa.

"Matarajio yangu makubwa ni kuona ninacheza soka la kulipwa katika ligi tofauti nje ya Zanzibar na Tanzania kwa ujumla, naamini malengo yangu yatatimia," Hilika aliongeza.

Alisema wakala wake anaendelea na mchakato wa kumtafutia timu nyingine ili abadilishe upepo baada ya msimu wa 2018/19 kupata nafasi ya kuitumikia klabu ya Bucavu inayoshiriki Ligi Kuu ya Jamhuri ya Kidemokrasia ya Congo (DRC).

Michezo

Ijumaa Mei 15, 2020

Nipashe



Martinez akaribia kutua Barca UKURASA 22



Katibu Mkuu wa Shirikisho la Soka Tanzania (TFF), Wilfred Kidao, jana alitoa ufafanuzi kuhusu mgao wa Sh. bilioni 1.1, ambazo shirikisho hilo limepokea kutoka katika Shirikisho la mchezo huo Duniani (Fifa). **PICHA: MAKTABA**

## Serikali yashikilia hatima Ligi Bara

**Na Mwandishi Wetu**

WADAU wa soka nchini wametakiwa kuendelea kuwa na subira kuhusiana na hatima ya Ligi Kuu Tanzania Bara, kwa sababu uamuzi wa mwisho utatolewa na serikali.

Katibu Mkuu wa Shirikisho la Soka Tanzania (TFF), Wilfred Kidao, alisema wamekuwa wakifanya kazi kwa karibu na serikali ili kuhakikisha wanapata ufumbuzi wa kumaliza ligi zote ambazo zimesimamishwa kutokana na janga la ugonjwa wa corona (COVID 19).

"Ninashukuru serikali yetu imekuwa karibu sana na sisi kipindi hiki, baada ya tamko la JPM (Rais John Pombe Magufuli), kuonyesha nia ya kurejesha ligi, tumekuwa na furaha sana kwa sababu malengo ya taasisi yatatimia, ni jambo jema, kurudi kwa ligi bado suala hili liko katika mamlaka za serikali," alisisitiza.

Alisema ikifikia muda muafaka TFF itatangaza tarehe mpya ya ligi na namna ligi hiyo itakavyochezwa. Alieleza hata Fifa imewataka wanachama wake wanaofanya uamuzi wa kurejesha ligi, ni lazima wafuate mwongozo wa serikali ambazo ndio zina wataalamu wa afya.

"Wadau watulie, wakiwa wanangoja vyombo vyetu vinafanyia kazi," Kidao alimaliza.

# UTATA MABILIONI YA FIFA WAFAFANULIWA

### TFF yafunguka fedha hizo hazikuletwa kujinusuru na corona, yaeleza ni mgawo wa...

**Na Somoe Ng'itu**

SHIRIKISHO la Soka Tanzania (TFF), limesema mgawo wa Sh. bilioni 1.1 walizopokea kutoka Shirikisho la Kimataifa la mchezo huo (Fifa), ni kwa ajili ya shughuli za uendeshaji na si kuzipatia klabu na wadau wengine kutokana na kuwapo kwa janga la corona (COVID 19).

**Mbali na klabu za Ligi Kuu Bara ambazo 'wanazitolea macho' fedha hizo, wadau wengine wanaohitaji mgao ni pamoja na Shirikisho la Soka Zanzibar (ZFF).**

Akizungumza jijini Dar es Salaam jana, Katibu Mkuu wa TFF, Wilfred Kidao, alisema fedha hizo ambazo wamepokea ni mgao wa kawaida wa shirikisho hilo, lakini Fifa wamezitoa mapema kabla ya muda wake uliopangwa awali.

Kidao alisema TFF ilistahili kupokea awamu hiyo ya pili ifikapo Julai mwaka huu, lakini kutokana na janga la COVID 19, Fifa iliamua kuwapa wanachama wake mapema ili kupunguza makali ya ukata yaliyosababishwa na ugonjwa huo unaotikisa duniani.

Katibu huyo alisema TFF haitatumia fedha hizo nje ya makubaliano na Tanzania imefanikiwa kuendelea kupokea mgawo huo kutokana na kutimiza vipengele vyote 10 ambavyo Fifa inahitaji kuona vinafanyika kwa nchi wanachama wake.

"Bila hata ya COVID 19, TFF ingezipata hizo hela, kwa sababu vipengele vyote 10 vinavyotakiwa vilikuwa vinakamilika, sisi tulikuwa hatuna wasiwasi, hii ni awamu ya pili ya mgawo, hatutakwenda nje ya matumizi yake na ukaguzi wake utafanyika kama kawaida," alisema Kidao.

Alisema pia lazima wawe na hesabu zilizokaguliwa na kupelekwa katika shirikisho hilo la dunia.

"Fedha hizi huwa haziji tu, huwa wanatoa Januari na Julai, lakini lazima ukidhi vigezo vya ukaguzi vya mwaka uliopita, ni fedha zinazoitwa za kusaidia shughuli za taasisi, kuna suala la mishahara, wakiwamo makocha (Taifa Stars na Twiga Stars), " alisema Kidao.

Alisema pia ili upate fedha hizo lazima uwe umeendesha kozi mbalimbali za waamuzi zisizopungua 10, Ligi ya Vijana, Ligi ya Wanawake yenye mechi 90 na itakayochezwa katika kipindi kisichopungua miezi sita pamoja na kuwa na Timu za Taifa za Wanawake mbili ambazo zimecheza mechi zaidi ya nane huku pia ukiwa na mfumo wa usajili unaotambuliwa na shirikisho hilo.

"Hizi fedha za Fifa hazina siri, na zina masharti makubwa, ukienda katika mtandao wa Fifa utakuta namna walivyoelekeza matumizi yake, na huwa wanafanya ukaguzi, kwa wale ambao wamefanya kazi na taasisi hizi kubwa wanajua namna hawa watu wanavyokagua kwa kupitia kila nyaraka zote... tena wanakuja nchini wakiwa na wakaguzi, napenda niwaambie kwa mwaka jana, Tanzania na Eritrea zilipewa sifa kwa jinsi zinavyotumia fedha zao," Kidao aliongeza.

Alisema Fifa huzitizama fedha hizi kwa ' jicho la pekee' ili kuhakikisha malengo yaliyokubaliwa yanatekelezwa kwa kiwango cha juu. Alisema fedha za Fifa zinakuja kutokana na mafanikio ambayo shirikisho hilo limeyapata chini ya utawala wa Rais, Wallace Karia ikiwamo kushiriki fainali za Kombe la Mataifa ya Afrika (AFCON), kuandaa fainali za vijana za Afrika (AFCON U-17) na kukata tiketi ya kushiriki Kombe la Mataifa ya Afrika kwa Wachezaji wa Ndani (CHAN) na kuna wakati Tanzania haikuwahi kupata mgawo huo.

Aliongeza fedha hizo za Fifa zitalipia madeni ya waamuzi waliochezesha mechi za Ligi Kuu ya Wanawake, Ligi Daraja la Pili huku wale waliochezesha Ligi Kuu Bara wakifuatia kulipwa madeni yao.

"Ukitumia vibaya fedha za Fifa unasimamishwa, masharti yake ili kurejeshwa ni magumu, ili kuyatimiza hamlali usingizi, tuache chokochoko, tunapoanza kuona mafanikio yanakuja, watu wakosoe kwa weledi na wasikosoe kwa chuki," alimaliza.

Aliongeza TFF inapitia changamoto mbalimbali lakini mwisho wa siku inapambana kuhakikisha inatekeleza vipaumbele vyake vya kuona soka la Tanzania linapata maendeleo.

GAZETI HILI HUTOLEWA NA KUCHAPISHWA NA THE GUARDIAN LIMITED, S.L.P 31042

9 770856 541002 >